MZALENDO KIMATHI

Ngugi wa Thiong'o
na
Micere Githae Mugo



AFR.
ALC.
PR
9381.9
N45
T7419
1978

19/52

S 18

Mzalendo Kimathi

WAANDISHI WA KIAFRIKA

S1 J.N. Somba: *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani*
S2 Ngugi wa Thiong'o: *Mtawa Mweusi*
S3 Ngugi wa Thiong'o: *Usilie Mpenzi Wangu*
S4 Peter Palangyo: *Kivuli cha Mauti*
S5 Bediako Asare: *Mwasi*
S6 Charles Ndibalema: *Fimbo ya Ulimwengu*
S7 Euphrase Kezilahabi: *Kichomi*
S8 Caleb Ogejo: *Mwindaji Hodari*
S9 Zani & Kitsao: *Mafarakano na Michezo Mingine*
S10 Ali A. Jahadhmy: *Kusanyiko la Mashairi (Anthology of Swahili Poetry)*
S11 Salim A. Kibao: *Matatu ya Thamani*
S12 Muwanga & Geranija: *Doa la Mauti*
S13 Ferdinard Oyono: *Boi*
S14 Ayi Kwei Armar: *Wema Hawajazaliwa*
S15 C. Omari: *Kuanguliwa kwa Kifaranga*
S16 Chinua Achebe: *Mwakilishi wa Watu*
S17 Chinua Achebe: *Mshale wa Mungu*
S18 Thiong'o & Mugo: *Mzalendo Kimathi*
S19 Obotunde Ijimere: *Kifungo cha Obatala na Michezo Mingine*
S20 Felix Osodo: *Hatari kwa Usalama*
S21 Nikolai Gogol: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*
S22 Peter Abrahams: *Mchimba Madini*

Ngugi wa Thiong'o & Micere Githae Mugo

MZALENDO KIMATHI

Kimetafsiriwa na

RAPHAEL KAHASO

HEINEMANN EDUCATIONAL BOOKS

NAIROBI

Kimetolewa na
Heinemann Educational Books (East Africa) Ltd.
Barabara ya Kijabe
S.L.P. 45314, Nairobi, Kenya.

© Ngugi wa thiongo & Micere Githae Mugo
© Tafsiri hii na Heinemann Educational Books (East Africa)

Kimetolewa mara ya kwanza katika Kiingereza na
Heinemann Educational Books (E.A.) Ltd.,
kama *The Trial of Dedan Kimathi*
Tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa kwanza 1978
Chapa ya pili 1981

Kimepigwa chapa na
General Printers Ltd.,
Barabara ya Homa Bay, S.L.P. 18001, Nairobi, Kenya.

PR
9381.9
N45
T7419
1978

SHUKRANI

Tungependa kumshukuru Karari Njama na wachapishaji wa kitabu cha *Mau Mau From Within* kwa kuturuhusu kunakili nakala yake ya 'Wimbo wa Kimathi'. Vilevile tungependa kusema kwamba ingawa makosa na udhaifu katika mchezo huu ni yetu sisi wenyewe, mchezo wenyewe unatokana na juhudi za pamoja ambapo watu wengi walitupa mashauri yao kwa moyo wao wote. Mengi ya mashauri yao tuliweza kuyatekeleza katika mchezo huu. Haiwezekani kuwataja majina yao wote, ila kusema kwamba mashauri yao yalitolewa kwa moyo wa uzalendo na moyo wa kuuchukia ubeberu.

UTANGULIZI

Mwezi wa Agosti 1971, ilikuwa mara yetu ya kwanza kukaa na kujadili mambo mengi tangu siku zetu za uanafunzi katika chuo kikuu cha Makerere ambapo tuliweza kushirikiana katika mambo mengi ya uandishi, na hata tukahariri kijigazeti kimoja kilichojulikana kama 'PENPOINT', kusoma na kutayarisha michezo ya kuigiza. Lakini sasa sote wawili tumeweza kuishi katika Amerika Kaskazini na kusafiri katika nchi za Ulaya magharibi. Baada ya kuushuhudia ubepari mahali ulipoanzia, tuliweza kutambua kwa yakini kwamba ubeberu ndio adui mkubwa wa wafanyakazi. Kwa mfano, huko Marekani ambako barabara zake hazina kifani, majumba makubwa yanayorambaramba mawingu, hali bora zaidi ya mawasiliano ulimwenguni, uvumbuzi mkubwa wa sayansi na ufundi, ama kila kitu cha anasa kinachoweza kumwingia mtu akilini; mbali na hayo yote kuna umaskini mkubwa kati ya Waamerika wa asili ya Kiafrika na wale wa kutoka Puerto Rico. Manufaa yote ya sayansi na ufundi, utajiri unaotokana na jasho la watu wengi, vyote vinaishia katika mifuko ya mabeperi wachache. Mbali na haya yote ilikuwa mipango mikubwa ya Marekani ya wizi kupitia kwa hila mbalimbali, mauaji na kuwafanya watumwa watu wa Afrika, Asia na Amerika Kusini. Amerika ilikuwa imeikalia Vietnam na Korea ya Kusini: vilevile Amerika ilikuwa ikiihudumia Afrika Kusini na Palestina. Kwa kweli, utajiri mkubwa wa Amerika ulipatikana kutokana na hatua ya kufukarisha maskini wengi.

Tulijadili juhudi za wazalendo wa Vietnam za kujikomboa kutoka katika ubeberu wa Kiamerika. Lakini tulikuwa na hakika kwamba wabeberu hao wangeshindwa siku moja. Jambo hili liliturejesha kwenye swala la Mau Mau, ambalo kwa kweli ndilo tulilokuwa tukilijadili. Je, swala la Mau Mau limeandikwa vya kutosha katika vitabu vyetu? Je hatua hii ya kishujaa iliyochukuliwa na watu maskini wa Kenya kupigana na serikali ya kibeberu ya Uingereza imepewa nafasi ifaayo katika vitabu vya fasihi vilivyoandikwa nchini Kenya? Kwa nini vitabu vyetu haviwezi kuonyesha kuwa wananchi waliweza

kubadili historia ya Kenya? Hebu tuwatazame mashujaa wetu: Kimathi, Koitalel, Me Kitilili, Mary Nyanjiru, Waiyaki. Kwa nini waandishi wetu, na watunzi wa mashairi, hawatungi nyimbo na mashairi ya kuwatukuza kwa vitendo vyao vya kukatalia mbali ubeberu? Watungaji wetu wa vitabu na mashairi wanaandika historia ya watu gani kwa vizazi vyetu vijavyo?

Hakuna kitabu chochote kilichoandikwa na Wakenya kinachoonyesha ujasiri wa watu wetu katika kupinga ubeberu na unyonyaji; jambo ambalo lilianza tangu karne ya kumi na tano na kumi na sita, wakati Wakenya na wananchi wengine wa Afrika Mashariki walipopambana na mabwana wa kikoloni wa wakati huo-majeshi ya Ureno ya kupigana, kuua na kuharibu mali za wananchi. Wanahistoria wetu na waandishi wetu wamekuwa na kazi nyingi wakikariri maandishi ya wakoloni yanayosema kuwa eti watu wetu hawakuwa na la kufanya ila kuzurura hapa na pale wakipambana wao kwa wao, na kwamba waliweza kufurahia utawala wa kikoloni wa Mwingereza! Sasa tujiulize. Waandishi kama hao wanaandika mambo hayo kwa manufaa ya nani? Hata wakiwa hawana haya, waandishi hao wameyasifu matamshi ya magavana wa kikoloni, ambao walikuwa wakifurahia jasho la Waafrika.

Sasa kwa nini kusiwe na mchezo kuhusu mashujaa hawa waliosahauliwa? Kwa mfano Kimathi? Ndiyo. Tulikubaliana kuwa tungeshirikiana kuandika mchezo kuhusu shujaa wa wananchi, Kimathi, na baadaye mchezo kuhusu Me Kitilili! Lakini tungeweza kufanya hivyo namna gani wakati ampapo mmoja alikuwa Kenya na mwingine New Brunswick? Tungeweza kufanya hivyo kwa barua. Lakini shauri hilo mwisho likaonekana halifai kutokana na umbali kati yetu na mambo mengine. Haikuwezekana mpaka mwaka wa 1974, wakati sote tulipokuwa walimu katika Idara ya Fasihi ya Chuo kikuu cha Nairobi, wakati ndoto yetu ilipokamilika.

Kuandikwa kwa kitabu hiki kumetupa fahari na mambo mengi. Tumeweza kujifunza mambo mengi katika historia ya kupambana na ubeberu na mambo yanayohusiana nao. Pia tuligundua kuwa Kimathi bado angali shujaa miongoni mwa wananchi. Kwa mfano siku moja, kwa msaada wa Bwana Mundia aliyetayarisha safari hiyo, tulitembelea mahali alipozaliwa Kimathi tukiwa na lengo la kujua habari

za Kimathi kutoka kwa watu waliomjua akiwa mtoto, mwanakijiji, na baadaye shujaa wa mapambano ya uhuru. Siku hiyo ilikuwa Jumapili na tulisafiri katika mabonde na milima na misitu iliyoweza kutukumbusha kuwa mahali hapo panapojulikana kama Karunaini palikuwa mahali ambapo mapambano yalikuwa makali zaidi. Karunaini ilikuwa karibu na msitu wa Nyandarua. Tuliposimama karibu na shule ambayo Kimathi alikuwa akifundisha, tuliweza kuona mahali ambapo Kimathi alipigwa risasi na majeshi ya Kiingereza. Mfereji mkubwa ambao wananchi walilazimishwa na wakoloni kuuchimba ili kuvitenga vijiji kutoka msituni ulikuwa bado unaonekana.

Kati ya watu waliosimama kuongea nasi alikuwa mwanamke mmoja aliyekuwa mwanafunzi wa Kimathi katika shule ya Karunaini; na wazee wanne ama watano waliomjua Kimathi tangu utoto wake. Je, nasi tulikuwa tumefika kupaona mahali alipozaliwa? Kutokana na watu hawa tuliweza kujifunza ukweli fulani kuhusu Kimathi, na vilevile mambo yaliyotofautiana. Kwa mfano inafikiriwa kwamba Kimathi alipigana katika vita vya pili vya ulimwengu. Na kwamba watu walifikiria kuwa vita hivyo ndivyo vilivyoweza kumfunza ujuzi wake wa vita pamoja na ujuzi wake wa kujitengenezea bunduki. Lakini ukweli ni kwamba Kimathi hakupigana katika vita hivyo hata kidogo. Aliweza kupata ujuzi wake wa vita kutokana na kuona mateso waliyofanyiwa wananchi. Watu wa Karunaini walimwonea fahari kubwa mwana wao. Walimsifu kama mwalimu mkuu aliyeweza kujitolea katika kazi yake, kama kiongozi wa kundi la michezo ya kuigiza alilioliita Gichamu, na mtu mwenye ucheshi mkubwa ambaye aliweza kuwafanya watu wengi kutiririkwa na machozi kwa kicheko. Walimsifu sana mtu huyu kwa wema wake mkubwa na upendo wake kwa watu wengine. Kweli alikuwa mwana wao mpenzi, kiongozi wao waliyemheshimu, na waliongea juu yake kama kwamba angali hai. 'Kimathi hatakufa kamwe' mwanamke akatamka. 'Lakini kama kweli ninyi watu mmemwua, twendeni mkatuonyeshe kaburi lake!' Alisema maneno hayo kwa sauti ya chuki na kutoogopa, na sisi kwa dakika mbili tatu tulikuwa kimya.

Tulirudi Nairobi tukiyafikiria maneno ya wale ambao walimjua Kimathi. Je, si wao wenyewe waliotuonyesha pale Kimathi alipopigwa risasi na kutiwa nguvuni? Je, hawakutuambia kuwa mama yake

Kimathi, ingawa alikuwa mwenda wazimu, aliruhusiwa kumtembelea mwanawe gerezani? Je, hawakutuambia maneno ya mwisho ya Kimathi yaliyokuwa katika taarifa iliyotolewa gerezani kwa siri-kwamba mapambano ya wananchi ya kujikomboa lazima yaendelee hadi utajiri na ardhi yote imerudishwa kwa Wakenya wenyewe? Kwa nini sasa uadui utokee wakati swala la kifo cha Kimathi linapotajwa? Lakini mioyo yetu ilijaa uchu wa kuendelea mbele. Tulidhamiria kutunga mchezo wenye uzito wa mtu yule tuliyehadithiwa na watu ambao hata hawakujua kuwa tungelikuja. Kitu kingine kilichotuzidishia uchu wetu ni kwamba vita vilivyoanzishwa na Kimathi vingali vikiendelea miongoni mwa watu wa Bara la Afrika ambao bado wananyanyaswa na ukoloni. Ilikuwa muhimu kwamba juhudi zote za mapambano lazima ziwekwe pamoja, kutoka wazungu waanze kuwasili nyakati za enzi za utumwa, juhudi za uhuru na demokrasia, mpaka mapambano ya kupigana na ukoloni mambo leo. Yote haya yangekuwa kufuatana na moyo ule wa mwanamke aliyetuambia kuwa Kimathi hangeweza kamwe kufa.

Kitabu cha Karari Njama *Mau Mau From Within* kilikuwa msaada mkubwa kwetu. Huyu alikuwa mtu ambaye alipigana na kuishi pamoja na Kimathi, na taarifa ya vita vya Mau Mau tunayopata kitabuni mwake ni tofauti kabisa na zile zilizoandikwa na Wakoloni, kama kitabu cha Henderson kinachojulikana kama *The Hunt for Dedan Kimathi*, ama kitabu cha Huxley kinachoitwa *A Thing to Love*, au vya Ruark vinavyoitwa *Uhuru and Something of Value*. Tulikubaliana kwamba jambo muhimu ni kuunda hadithi yetu tukitia maanani juhudi za Mau Mau na Kimathi, pamoja na mapambano ya wananchi kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Mchezo huu si maigizo ya kesi ya bandia huko Nyeri, bali ni juhudi za wananchi za kuvunjilia mbali utawala wa miaka sitini chini ya ubeberu wa Kiingereza, na juhudi zao za kuendelea kupinga unyonyaji, udhalimu, na mambo mengine ya kuteka akili.

Katika jambo hilo, tunaamini kuwa maandishi yote ya Kenya, na waandishi wake lazima wahusike. Ni lazima tuwe upande wa wananchi ama upande wa Ubeberu. Waandishi wa Kiafrika wanapigana na ubeberu ama wanasaidia kuuendeleza. Tunaamini kuwa mchezo mzuri wa kuigiza ni ule unaounga mkono juhudi za wananchi na

kuwasahihisha makosa yao na kuwatia moyo kuendeleza maendeleo mbalimbali kwa manufaa yao. Kwa hivyo lengo letu ni wananchi wanaowakilishwa na Kimathi kama wajenzi halisi wa historia ya Kenya.

Ngugi wa Thiong'o
Micere Githae Mugo

Nairobi, Agosti, 1976

Wahusika

KIMATHI WA WACHIURI

NJAMA

MATENJAGWO

MBARIA KAHIU *Majemadari*

KIMEMIA

OLE KISIO

MWANAMKE

MVULANA

MSICHANA

SHAW HENDERSON

Huyu pia anaweza kuchukua mahali pa Hakimu, Mwendeshaji wa mashtaka, n.k.

WAITINA - *Askari mzungu ama Mkuu wa Wilaya*

ASKARI WA KWANZA

JOHNNIE

ASKARI WA PILI

ASKARI WA KWANZA WA KIINGEREZA

ASKARI WA PILI WA KIINGEREZA

ASKARI WA K.A.R

WALINZI

MLINZI WA GEREZA

MLOWEZI

MWANAMKE MZEE WA KIZUNGU

GAKUNIA *ama kwa jina jingine* GATOTIA

PADRI

MKURUGENZI WA BIASHARA

MWANASIASA

WENYE MABENKI - MZUNGU, MWAFRIKA, MHINDI

HUNGU

MWENDANDA *Wasaliti*

GATI

GACERU

WAMBARARIA

UMATI NA WAPIGANIA UKOMBOZI 1,2,3,4 na 5.

UTANGULIZI

Mahakamani. Hakimu wa kiingereza anaongoza mashtaka. Karibu sana na pale alipoketi, ni karani wa Kiafrika anayeonekana nadhifu. Anachezacheza na makaratasi yaliyo hapo mezani. Kimathi ambaye amefungwa pingu yuko kizimbani. Wanaomlinda ni Waitina-Mkuu wa Wilaya mweupe ambaye pia ni afisa wa polisi-na askari wawili wa Kiafrika wa jeshi la K.A.R. Wote hao wamebeba silaha. Mahakama imejaa watu kupita kiasi. Waafrika wamesongana upande mmoja wa mahakama wakikalia viti vya mbao. Upande wa pili wa mahakama wazungu wanaonekana wameketi kwenye viti vizuri visivyoumiza.

Ni kimya kabisa

HAKIMU: Dedan Kimathi bin Wachiuri, au kwa jina jingine Waziri Mkuu ama *Jemadari,* asiye makao maalum, unashtakiwa kwamba usiku wa Jumapili ya tarehe 21 mwezi wa Oktoba, mwaka 1956, ukiwa Ihururu ama karibu na hapo, ulipatikana ukiwa umebeba bunduki aina ya *revolver,* bila leseni, kinyume cha kifungu 89 cha sheria za nchi hii, jambo ambalo kulingana na hali ya hatari iliyopo nchini, ni kosa la jinai. Je, wakiri ama wakana mashtaka hayo?

[Kimathi anabaki kimya bila kujali.]

Ningependa kukutahadharisha kwamba kimya chako chaweza kuchukuliwa kwamba unadharau mahakama, na hapo inaweza kunilazimu niamuru utiwe ndani kwa kifungo cha muda fulani.

[Kimathi anabaki kimya. Kuna mnong'ono mahakamani. Hakimu anagonga meza kwa nyundo.]

Kila mtu kimya mahakamani! Nitarudia mashtaka. Dedan Kimathi, unashtakiwa kwamba usiku wa Jumapili ya tarehe 21 mwezi wa Oktoba, mwaka wa 1956 ukiwa Ihururu ama karibu na hapo, ulipatikana ukiwa umebeba bunduki aina ya *revolver,*

bila leseni, kinyume cha kifungu cha 89 cha sheria za nchi hii, jambo ambalo kulingana na hali ya hatari iliyopo nchini, ni kosa la jinai. Je, wakiri ama wakana mashtaka hayo?

Kimya kwa sekunde chache. Halafu giza.

ONYESHO LA KWANZA

Kiza tititi. Midundo ya ngoma inasikika kwa mbali, lakini inaendelea kuwa na sauti kubwa mpaka mwisho hakuna sauti nyingine isipokuwa midundo hiyo ya ngoma. Baadaye midundo hiyo inaanza kufifia mpaka sauti za watu zinasikika.

Mapambazuko yanaingia.

Wananchi wanasikika wakiimba nyimbo zinazodhihirisha moyo wao wa kutaka kumwondolea mbali mtu mweupe. Nyimbo zao zakariri historia yao ya mapambano ya uhuru.

Tutanyakua mashamba yetu
Tupiganie uhuru wetu
Tuikomboe elimu yetu
Tutanyakua viwanda vyetu
Utamaduni ni mashamba yetu
Damu na jasho zatiririka
Tutakomboa udongo wetu!

Risasi inapigwa hewani. Kunakuwa giza. Ngoma na sauti zinakoma. Katika kimya hicho, kunasikika mlio wa maumivu wa mtu fulani, ukifuatiwa na vilio vya huzuni. Viboko vinasikika vikitandika miili ya watu. Halafu kunafuata kilio kikali na makelele ya maumivu. Kunakuwa kimya. Halafu mwangaza unaanza kutokeza polepole jukwaani, huku mlio wa ngoma ukianza kusikika. Nyimbo za huzuni zinasikika huku maigizo ya Historia ya Mwafrika yanapofanywa katika jukwaa. Maonyesho hayo yako katika sehemu nne, na yaendelea bila kutatizwa.

Sehemu ya I: Katika sehemu hii anaonyeshwa Chifu wa Kiafrika anayeuza watu wake na kupewa bidhaa na mfanyi biashara ya utumwa mweupe. Waafrika kadha wanaume wenye nguvu, na

wanawake wachache wanakabidhiwa mzungu, na badala yake, Chifu wa Kiafrika anapewa nguo na shanga. Jamaa za wale waliouzwa utumwani wanalia na kujitupa chini, na wengine wanakunja ngumi kwa hasira.

Sehemu ya II: Kundi la watumwa waliofungwa pamoja linaingia katika jukwaa wamebeba mizigo mizito. Wanapiga makasia ndani ya mashua, huku wakitandikwa na mabwana zao wapya.

Sehemu ya III: Wafanya kazi wa Kiafrika, wanaofanya kazi katika shamba la Mzungu wakisimamiwa na mnyapara wa Kiafrika asiye na huruma. Mwenye shamba anajitokeza na kuchunguza kazi hiyo inavyofanyika.

Sehemu ya IV: Maandamano makali ya Waafrika wasio na woga, wakiimba nyimbo za kupinga ukoloni yanaonekana.

KIONGOZI: Tumalize udhalimu!
Tuwakomboe watu wetu!
UMATI: Tumalize udhalimu!
Tuwakomboe watu wetu!
WIMBO: Tutanyakua mashamba yetu!
Tutakomboa Afrika yetu!
Tutanyakua viwanda vyetu!
KIONGOZI: Tumalize udhalimu!
Tuwakomboe watu wetu!
UMATI: Tumalize udhalimu
Tuwakomboe watu wetu!
KIONGOZI: Tukomeshe mauaji!
UMATI: Tukomboe watu wetu!
KIONGOZI: Ndugu zangu tutavunja-
UMATI: Minyororo ya wanyonyaji!
KIONGOZI: Tushikeni bunduki!
UMATI: Tuijenge nchi mpya!
WIMBO: Kupigwa na kufungwa jela
Hakutatuzuia sisi wananchi
Kunyakua uhuru wetu
Na mashamba yetu

Milio ya risasi inasikika. Ngoma zinazidisha midundo yao.

SAUTI CHACHE: Uhuruuuuuuuu-uu!

Kimya.

Sasa mwangaza kamili unaingia katika jukwaa, mpaka inakuwa rahisi kutambua watu wanaopitapita kwenye jukwaa. Wengi wa wale wanaokimbia wamevaa chupi tu. Kwa muda mchache wanaonekana askari wawili wa Mau Mau wakishika zamu wakiwa na bunduki. Karibu na jukwaa panaonekana kichaka. Pia karibu na barabara yanaonekana mawe makubwa. Wengi wa wale wanaokimbia wanapita katika jukwaa na kutokomea upande wa pili.

Karibu na jukwaa kunasikika milio ya viboko vinavyochapwa watu, ama milio ya mateke ama ngumi.

Wanatokeza Waitina, akiwa na Gakunia-Gatotia amejifunika.

WAITINA: *[akiwaamuru askari wawili walio upande wa pili wa jukwaa]:* Askari, lindeni vizuri barabara na wapigeni risasi magaidi. Sikia?

ASKARI WA PILI: Ndiyo Afande.

Askari wa kwanza hakuitikia!

WAITINA: Askari.

ASKARI WA PILI: Afande!

WAITINA: Wachukue wale magaidi wa Mau Mau na uwapange kwenye msitari wawiliwawili.

ASKARI WA PILI: Tayari Bwana!

WAITINA: Wapeleke katika sehemu ya kuchunguzwa. *[anamwota askari wa kwanza]:* Yeye anaweza kulinda barabara. Na mwambie aamke, kwa jina la Yesu! Umesikia?

ASKARI WA PILI: Ndiyo Bwana.

Misitari miwili ya wananchi inaonekana. Askari wa pili anajaribu kuwafanya watembee kiaskari.

WAITINA: *[amejitokeza ghafla]:* Tembeeni vizuri! Pesi! Na pana kimbia. Weka mikono yenu vichwani. Haraka! Tembea! *[askari wa pili anageuka na kurudi mbio]:* Ngoja!

Watu wanasimama wakiwa hawajui yaliyosemwa. Hawakujua ikiwa amri hiyo walipewa wao ama vipi. Wanasukumwa na kupelekwa mbele ya Waitina anayewatazama vikali. Gakunia ambaye ni msaliti anawatazama.

WAITINA: Leta karatasi yako.

MTU WA KWANZA: Sina.

WAITINA: *[anampiga teke]:* Sina afande! Rudia!

MTU WA KWANZA: Sina Afande.

WAITINA: Kazi yako?

MTU WA KWANZA: Kulima.

WAITINA: Mtu ya Kimathi?

MTU WA KWANZA: Hapana. *[Waitina ananyosha bunduki yake kama kwamba angempiga na tako la bunduki hiyo, lakini mara mtu wa kwanza akakumbuka kosa lake na kuongeza]:* Afande. *Msaliti anaitikia kwa kichwa kwamba mtu wa kwanza si mfuasi wa Kimathi.*

WAITINA: *[akimsukuma mtu wa kwanza bila huruma]:* Kwenda. Utajibu maswali zaidi katika uwanja wa maulizo, mwanaharamu mweusi! . . . Na wewe?

[Gakunia ananyosha mkono kumwita mtu wa pili aliyevaa shati jekundu, na ambaye amebeba kikapu cha matunda.] La. Si wewe. Wewe na shati nyekundu.

MTU WA PILI: Mimi?

Waitina anamnyakua kikapu na kuangalia ndani yake.

WAITINA: Unafanya kazi wapi? Unabeba nini kikapuni?

MTU WA PILI: Mimi ni mwuzaji matunda. Kila siku huimba: "Machungwa leo ni rahisi".

WAITINA: *[hawezi kuzuia kicheko. Halafu anachukua machungwa machache na kuyarusha yale mengine kwa kukirusha kikapu chenyewe]:* Nenda ukachunguzwe zaidi. Lazima uende Manyani ukayauze machungwa yako huko.

[mwenye machungwa anauma vidole vyake na kutaka kuyarudisha machungwa kikapuni, lakini Waitina anamkemea.]
Kwenda pesi! Wote kwenda

Msitari wa wananchi hao waliotiwa nguvuni unapitia kwenye jukwaa. Mtu wa pili anaonekana mwenye wasiwasi kama kwamba alikuwa akitazamia kumwona mtu fulani lakini akakosa kufanikiwa kufanya hivyo.
Sasa ni alfajiri na mwangaza umesambaa pote katika jukwaa. Mwanamke anaonekana akitembea katika jukwaa. Umri wake ni wa kati ya miaka thelathini na arobaini, lakini uso wake unamwonyesha kuwa mwanamke mwenye dhamira kubwa. Sura yake yavutia. Amevaa nguo za wanawake wa shamba, na miguu yake haina viatu. Ingawa anaonekana kama mwanamke yeyote wa kawaida, mwanamke huyu anaonyesha kuwa anajua mambo mengi ya ulimwengu, na kufahamu hali ya ujamaa wa Kiafrika. Katika vitendo vyake vyote anaonekana mwanamke mwenye akili ambayo iko chonjo daima.
Anaonyesha kuwa hajali hatari yoyote, na majibu ya maswali anayoulizwa yanaonyesha kuwa yu madhubuti sana katika dhamira yake. Anaonekana kuwa ni mama na mpigania ukombozi pamoja. Amevaa leso iliyofungwa katika rinda lake alilovaa, amebeba kikapu kilichotengenezwa kwa katani. Anatembea kwa uangalifu kana kwamba anatembea katika ardhi iliyo hatari kwa usalama wake. Anapotembea anahamaki kuona ameelekezewa mtutu wa bunduki.

MWANAMKE: Uuu-u! Nduri ici ni kii giki?
Anarudi nyuma lakini bunduki inamfuata. Mtu mweupe, aliyevalia kivita anamfuata.
JOHNNIE: Simama kabisa. Vizuri. Toa passbook.
MWANAMKE: Ati pasi?
JOHNNIE: Ndiyo, passbook. Wapi passbook?
MWANAMKE: Sina.
JOHNNIE: Sema Afande.
MWANAMKE: [kwa dharau]: A-fa-nde-ee
JOHNNIE: Sina, Afande.

MWANAMKE: Sina Afande *[anasema kwa sauti ya dharau, ambayo inaweza kuwa na maana kuwa, "sina mtu anayeitwa afande."]*

JOHNNIE: Kuja! Njoo hapa. *[Mwanamke anasimama bila kufanya lolote. Ni huyo askari anayemzunguka. Anazunguka kiasi cha kuwa hawezi kukiona kikapu. anamtazama mwanamke kila mahali. Kwa ncha ya bunduki anamfunua nguo kana kwamba anataka kutazama miguu yake. Lakini mwanamke huyo anajiondoa kwa utaratibu. Anamaliza kumkagua na kuitikia kwa kichwa chake kana kwamba amependezwa na mwanamke huyu. Sasa anajichekelea kwa kutamani kumpata mwanamke huyu.]* Si mbaya. Miguu mizuri, eh? Uso wa kuvutia, eh? *[Karibu anapumzika, na hata kuwa tayari kuweka chini bunduki yake, lakini mara anasikia sauti kutoka upande wa pili:*

"Laini!" – mlio wa kiboko. "Laini." Anatazama upande huo unaotoka sauti, na kurudia hali yake ya mwanzo ya ukali.] Mbona hivi? Kwa nini wewe hapana passbook? Passbook yako wapi?

MWANAMKE: Mimi? Wanawake hawabebi *passi.*

JOHNNIE: *[anatazama kwa mara nyingine. Anatulia. Anaitikia kwa kichwa kuwa mwanamke huyo anamfaa]:* Wanawake wenyewe ni passbock, eh? Hata mbinguni. *[anachekelea kwa mapenzi]:* Unaishi sehemu hizi? *[Lakini kabla mwanamke hajajibu, Johnnie anageuka hali yake, na anaonekana ametishika. Anaweka bunduki yake tayari na anarudi nyuma hatua mbili kutoka kwa mwanamke.]* Ni nini? Kile ni nini? Mkoba unaobeba una nini? *[kwa ukali]:* Toa! Toa! Weka chini, upesi!

MWANAMKE: Hiki? *[anamwonyesha askari kikapu akijifanya ameshangaa.]*

JOHNNIE: Kiweke chini.

MWANAMKE: Lakini ni kikapu tu. Mkoba mdogo unaotumiwa na wanawake kubebea vitu vyao.

JOHNNIE: Kiondoe kichwani, nasema. Naam, namna hiyo. Kiweke chini. Naam, namna hiyo. Sasa weka mikono yako kichwani. Rudi nyuma, hatua mbili. Naam, hivyo ni vizuri. Usijaribu kufanya visa vyovyote. *[anakikaribia kikapu kwa uangalifu huku akimtupia jicho mwanamke.]*

MWANAMKE: *[pia ameogopa, lakini anajifanya kuwa hakuogopa. Ili kumfanya asiendelee kukagua kikapu hicho, mwanamke anaanza mtindo wa kuongea upesiupesi.]*

MWANAMKE: Unaogopa? Bwana mweupe unaogopeshwa na skati ya mwanamke? Bwana mweupe unaogopeshwa na kikapu cha mwanamke cha shamba na cha kubebea vitu?

JOHNNIE: *[akichukua kikapu]:* Huwezi kujua kilicho katika vitu hivi vya kishenzi.

Anavimwaga vitu vyote vilivyo katika kikapu hicho. Mwanamke ameogopa lakini anajifanya kuwa hakuogopa hata kidogo. Ndizi, machungwa, viazi vitamu na kasha lililofungwa katika karatasi vinamwagika. Wakati huohuo mwanamke anaongea harakaharaka akitaka kumfanya askari huyo asiendelee na kazi hiyo.

MWANAMKE: Nisingeweza kuamini, kwamba askari mweupe kama wewe angeweza kuogopeshwa na. . .

JOHNNIE: Aaaa, kumbe ni ndizi tu. . .

MWANAMKE: Nitawatobolea siri hii watu wote mtaani . . .

[Johnnie anachekelea, halafu anachukua ndizi, anaiambua na kuila, huku akijaribu sana kuficha hofu yake ya hapo awali]: Na unakula ndizi pia! Ni asubuhi iliyoje! Asubuhi ya maajabu. *[akitaka kumjaribu askari]:* Naweza kuondoa mikono yangu kichwani sasa?

JOHNNIE: Bila shaka. Mtu mweupe pia hushikwa na njaa. Hasa baada ya usiku mzima bila chakula wala usingizi. Ilinibidi kupambana na maharamia wale hadi alfajiri. Hii *[anakula ndizi nyingine]:* ilikuwa ni hatua ya tahadhari, na hata hivyo pengine ungekuwa umebeba bunduki. Unaonekana kama Mau Mau. Kama mmoja wa wanawake wafuasi wa Kimathi. Mmoja wao anayeitwa Wanjiru alikuwa mwembamba na mwenye nguvu. Alipigana katika vita vya *Beehive* kama simba. Si ajabu kuwa maharamia walimpa cheo cha Kanali. *[karibu ajisahau kuwa ni askari na yuko kazini]:* H'm. Ungemwona aliposhikwa ndiyo ungaliamini ninayosema. Alitutukana na kututemea mate na kutupiga mateke tulipokuwa tukimfunga. Halafu alipokuwa katika kambi ya Karunaini, alikataa kula ama kunywa chochote.

Na akakataa kutuambia tungalipompata Kimathi. Na si hivyo tu, aliniuma kidole.

Unajua kwa nini aliniuma? Kwa sababu nilitaka kuthibitisha kama kweli alikuwa mwanamke.

Waafrika walio katika upande wetu, Gati, Hungu, Mwendanda na hata Wambararia, kaka yake Kimathi, walimwogopa mwanamke huyo. *[Sasa anaokota kikasha na kuanza kukifungua. Mwanamke anaanza kuzungumza harakaharaka.]*

MWANAMKE: Hata hivyo ni jambo lisilo la kawaida. Wanaume wetu hawaogopi wanawake. Hawaogopeshwi na . . . na. . . .

JOHNNIE: Aaah. Kumbe ni mkate tu. Ha ha ha! *[baada ya kuushika mkate anajiwa na mawazo mengine]:* Ni mkate mzito sana. Ni mkate wa wimbi kutoka mwituni? Unaweza kuwa kombora. Maharamia wana njia nyingi sana. Hata wanayo mabunduki yaliyotengenezwa majumbani! Wenda wazimu! Nionje kidogo?

Anafanya kama atakayeuvunja vipande viwili. Mwanamke anapiga magoti, karibu amfikie miguu yake. Askari anaogopeshwa na hatua hiyo. Anarudi nyuma kidogo, anauweka chini mkate na kumshikia bunduki mwanamke. Lakini hata hivyo mwanamke huyo anazungumza bila kuchoka.

MWANAMKE: *[huku akifanya kitendo cha hapo juu]:* Usiule, Bwana. Bwana mkubwa. Afande mara mia. Ndicho tu kitu nilichonacho kumnyamazisha adui anayetumaliza.

JOHNNIE: Adui?

MWANAMKE: Njaa. Kama ukiula, nitakufa. Nilichukua muda mrefu kukanda unga wa wimbi. Angalia, wewe sasa umemaliza karibu ndizi zangu zote. Unastahili kufa. Mwonee huruma mwanamke maskini kama mimi.

JOHNNIE: *[Akiwa na huruma kutokana na malalamiko ya kike. anaonekana ametosheka na maelezo hayo. Hajui kwamba mwanamke huyo anajifanya.]*

Huonekani maskini hata kidogo. Simama. Unachotaka ni brashi, maji, sabuni, viatu vya kisasa. Hapo umekuwa mwanamke wa kisasa.

MWANAMKE: Bwana, mimi ni mwanamke maskini. Niache niende

zangu. Mimi ni mwanamke maskini anayewachukulia chakula watoto wake wanaokufa kwa njaa.

JOHNNIE: *[akimkaribia, anamchezea kama atakayemgusa mwanamke]:* Ni wanawake maskini kama wewe wanaowapelekea chakula maharamia wa Mau Mau msituni, eh? *[mwanamke anarudi nyuma]:* Mume wako yuko wapi?

Kabla mwanamke hajajibu, kuna sauti ya nyayo; Johnnie anaogopa na kunyakua bunduki yake na kuanza mbio. Anapomkumbuka mwanamke anatazama nyuma na kumkonyezea, halafu anatoweka. Mwanamke naye anafanya ishara ya dharau, anatazama hapa na pale akitaka kujua sababu ya kelele hizo, na anapogundua kwamba hakuna mtu atokeaye, anaanza kuokotaokota vitu vyake vilivyotapakaa. Anauweka mkate kikapuni kwanza. Halafu anakusanya viazi vitamu. Anapokusanya viazi anasikia sauti ya askari wa K.A.R. wakikaribia. Anachukua karatasi iliyokuwa imefunga mkate na kuokota machungwa machache, na kuyasahau mengine. Anajificha katika kichaka cha karibu muda mchache kabla ya askari kuwasili.

ASKARI WA KWANZA: *[akiwa amekasirika]:* Wako wapi maharamia ambao walisemekana wako kila mahali huku Nyeri? Tumekuwa macho usiku mzima bila kuona hata mmoja wao. Jambo tunalofanya ni kuwasumbua watu wasio na hatia. Jinsi mzungu anavyotufanya tutamani kuuana ni jambo la kushangaza!

ASKARI WA PILI: *[bila kujibu swala lililoulizwa na mwenzake]:* Bloodyfuckin' Mau Mau wamemalizwa bila haramia mwenyewe Kimathi!

ASKARI WA KWANZA: Sasa ina maana gani kuwatia nguvuni wana kijiji wote?

ASKARI WA PILI: *[akinuna]:* Kuhojiwa. Watu hawa ni wajanja bwana. Ndio hao walioshambulia kituo cha kizuizi jana usiku wakijaribu kumwokoa Kimathi. Lakini watakiona cha mtema kuni. Kiongozi wao wa uharamia anafikishwa mahakamani Nyeri leo leo mchana. Kesi yake itasikizwa barabara, siyo kama zile wanazoendesha msituni. Sasa waona jinsi mzungu anavyofanya mambo ya haki?

ASKARI WA KWANZA Niulize kesho kama leo hakutakuwa na jaribio la kumwokoa. Kama ilivyotokea jana.

ASKARI WA PILI: Mimi binafsi sifikiri watajaribu tena. Hawa Mau Mau ni waoga kupita kiasi. Hawawezi kujitokeza hadharani na kupigana kama wanaume wafanyavyo.

ASKARI WA KWANZA: Mara nyingi wamefanya hivyo. Kama serikali inataka kuepukana na shida, ni lazima ichukue hatua. Lazima ihakikishe kuwa wale wanaowaunga mkono maharamia wako mbali iwezekanavyo.

ASKARI WA PILI: Nilikuwa nikifikiri sasa hivi, kuwa uliuliza ni kwa nini wananchi wasio na hatia walikuwa wakichukuliwa mateka.

ASKARI WA KWANZA: Kuchukuliwa mateka na kuwekwa mbali, ni mambo mawili tofauti kabisa.

ASKARI WA PILI: Wewe wafikiri mzungu ni mjinga. H'm. Hivi tunavyozungumza Gatotia, Gaceru, Gati, Mwendanda na Wambararia, kaka yake Kimathi mwenyewe, wamevikwa shela, na wanawasema maharamia na wafuasi wao mmoja mmoja. Mimi binafsi naogopa jambo tofauti kabisa. Wanawake wenye hasira, ambao wamepoteza waume zao na watoto wao wanaweza kumrarua Kimathi vipande vipande.

ASKARI WA KWANZA: Wapi? Hivyo ndivyo Bwana Shaw Henderson anavyosema lakini hawajui wananchi. Kimathi ni bingwa wa wananchi. Wanampenda kuliko kitu chochote, upende usipende.

ASKARI WA PILI: *[kwa wasiwasi]:* Unaongea kama mmoja wa maharamia bwana.

ASKARI WA KWANZA: *[akiwa amekasirika]:* Unasemaje?

ASKARI WA PILI: *[akimbembeleza]:* Bloody bugger. *[anampigapiga mabegani]:* Usikasirike bwana. Hiyo ni dhihaka ya askari. Lakini hebu nikuambie, kuwa baada ya kesi, baada ya Kimathi kunyongwa, hakutakuwa na mapigano zaidi. Utakuwa ndio mwisho wa vita vya Mau Mau. Mzungu! Usimchezee.

ASKARI WA KWANZA: Si neno, tutaona.

Kwa mbali kunasikika milio ya magari.

ASKARI WA PILI Haraka, magari yanaondoka.

[lakini mara anaona machungwa yaliotapakaa]: Hebu angalia! Hii ni dalili kuwa Mau Mau hawako mbali.

ASKARI WA KWANZA: Kwani watu wengine hawali machungwa? Fanya haraka tuyakute magari kabla hayajatuacha nyuma.

[Wote wawili wanaondoka kiaskari.]

MWANAMKE: *[Anajitokeza kutoka alipokuwa amejificha]:* Wui, nimeponea tundu ya sindano. Niliokoka kutoka kucha za chui na kuangukia mdomo wa simba. *[anaanza kuokota tena machungwa yaliyotawanyika]:* Mmoja wa hao askari alisema kitu gani? eti 'jinsi mzungu anavyotufanya tupende kuuana ni jambo la kushangaza'. Na kwa kweli alisema kweli tupu. Ni lazima awe mmoja wa watoto wetu wapotevu. H'm. Hebu tutazame hali yetu sisi wakulima wa vijishamba vidogo tulivyoachiwa na mzungu. Tunaambiwa kuwa, wewe u Mjaluo, wewe u Mkalenjin, wewe u Mkamba au Mmasai ama Mkikuyu. Wewe ni mwanamke na wewe u mwanamume. Wewe u hivi na wewe u vile.

[baada ya kufikiri]: Ndiyo, sisi ni kama chungu tunaokanyagwa na ndovu wasio na huruma.

Huku akiwa na huzuni, mwanamke anavuta jiwe la kuketia katika jukwaa, huku akiimba. Anaendelea kupanga vizuri mali yake kikapuni, akiufunga mkate kwa uangalifu.

WIMBO: Bururi uyu witu andu airu
Ngai ni aturathimiire
Na akiuga tutikoima kuo
[ama wimbo mwingine unaofaa kwa wakati kama huu.]

Mlio wa ndege unasikika. Mwanamke anatazama juu. Anaendelea na kazi yake.

MWANAMKE: Haya ni majaribio ya nguvu zetu
Majaribio ya imani, matumaini na juhudi zetu
Majaribio ya uaminifu wetu
Haki zetu
Lazima nimpate muuzaji matunda mara moja

Lazima pia nijihadhari na mitego zaidi ya adui.

Anamaliza kufunganya mzigo wake. Anapokuwa tayari kuondoka mara wanaingia mvulana mkubwa aliyevaa matambara akimfukuza msichana. Msichana anaonekana bado kijana sana, lakini bila shaka ameona malimwengu. Hao wawili wanakimbia kupita jukwaa, halafu wanarudi. Mvulana anamkamata huyo msichana na wote wawili wanaanguka jukwaani. Mvulana anapomkamata msichana, anaanza kupiga kelele.

MVULANA: Ziko wapi?
Ziko wapi pesa zangu?
Nitakuulia mbali usipozitoa.

Mwanamke anawaendea na kumwondoa mvulana. Bila shaka mwanamke ana nguvu kwani anaweza kumshika kila mmoja wao kwa mkono mmoja wasiweze kukaribiana.

MWANAMKE: Mvulana mzima kama wewe, si aibu hii? Tena wataka kumuua dada yako! Binti yà mama yako!

MVULANA: Dada yangu? Si dada yangu. Si dada ya mtu yeyote. Ni mwizi!

MSICHANA: Usiniite mwizi, wewe jahili. Mimi si mwizi.

MWANAMKE: Amefanya nini?

MSICHANA: Sikufanya kitu . . . *[analia]* yeye . . . *[analia]* ni mchokozi tu, ananionea.

MVULANA: Wasema hukufanya kitu! *[akijaribu kujitoa kutoka mkono wa mwanamke]:* Ngoja nimpate nimwonyeshe kuwa amenifanyia uhasama mkubwa.

MWANAMKE: *[akiwa na hasira za mzazi]:* Hutapata chochote kwa kujaribu yale unayotaka kumfanya. Ni lazima uwe na roho ya kibinadamu wala si roho ya kinyama kama hivyo ulivyo.

MVULANA: *[akiwa na hasira]:* Mwongo, malaya. Ni lazima anilipe pesa zangu. Ama atakiona.

MSICHANA: Puuu. *[atema mate. Mvulana anataka kumshika, lakini anazuiwa na mwanamke. Lakini msichana anajitahidi mpaka anajitoa mkononi mwa mwanamke na anatoweka. Mvulana anataka kumfuata lakini anazuiliwa barabara na mwanamke.]*

MVULANA: *[akiwa amekasirika kwelikweli]:* Umefanya atoweke. Wewe ni mwanamke mbaya. Lakini hata hivyo nitampata tu.

MWANAMKE: *[anamshika mabega na kumsukasuka]:* Wewe ni mtoto wa mwanamke? Natamani kukuvunja shingo. Unakimbia hapa na pale kumfukuza msichana na hali unaelewa kuwa magari ya adui yanazunguka kila mahali Nyeri kuwatafuta wapigania uhuru? Moyo wako ukoje wewe? Huwezi kuona sasa umekuwa mtu mzima? Na kwamba unaweza kupelekwa Manyani kuzuiliwa? Wamkimbiza msichana namna ile, kwani amefanya nini? *[mwanamke anamwachilia, halafu anamtazama kwa jicho la kumlaumu. Mvulana anaonekana pia anaogopa]:* Sijapata kukuona mahali popote?

MVULANA: *[ananyamaza na kuanza kumwangalia mwanamke. Uchungu na hofu vinamkabili, na bila yeye kujua afanyavyo, anaanza kutoa hadithi yake]:*

Wajua, ilikuwa ni katika mji wa Nairobi. Yeye, mimi na wavulana wengine na wasichana tulikuwa tukizurura katika mitaa na barabara za mji *[Mvulana anakatiza maongezi yake, anamwangalia tena mwanamke na kuangalia chini.]*

MWANAMKE: Usiwe na hofu sasa. Keti hapa. Ndiyo, ulisema ulikuwa mkizurura barabarani. Ni barabara zipi?

MVULANA: Eastleigh, Pumwani, Shauri Moyo, Bahati, Makadara, katikati ya mji: Delamere Avenue, Herdinge, Kingsway, Queensway, Government Road, kila mahali.

MWANAMKE: Ehee!

MVULANA: *[akianza kufurahia hadithi yake]:* Tulichokora kila pipa la taka kutoka Grogan hadi Kariobangi. Lakini mara nyingi tulidowea katika hoteli kubwa kubwa: New Stanley, Norfolk, Grosvenor. Kulikuwa na watalii na makabaila wengi, na tulikuwa tukiwabebea mizigo yao. Wakati mwingine tulijifanya viwete ama vipofu na viziwi. Waliweza kutupa pesa, na hata mara nyingine shilingi kumi! Polisi walituvamia lakini tukaweza kutoroka.

[Anasita.]

MWANAMKE: Endelea!

MVULANA: Basi siku moja, mimi na msichana huyu tulikuwa tumeketi nje ya New Stanley. Tulipokuwa tukizungumza, pakatokea

Mwamerika mmoja mnene aliyekuwa amebeba mizigo mizito. "Saidia masikini Sah,
Me and my sister
can carry your bags."
[akiigiza maumbile ya Mwamerika pamoja na maongezi yake na pia akiigiza vile walivyopewa mizigo na huyo Mwamerika kubeba.]
"Here, you take this boy. And your sister can take this, okay? Good boy."
[mvulana anajaribu kutembea, akijifanya kama mtalii]: "A beauddiful country . . . beauddiful ciddy and beauddiful people eh?"
[anajifanya anachukua kamera begani na anapiga picha]: "Take the baggage to that taxi over there. Understand? Good."
[mvulana anarudi nyuma hatua chache, halafu anasimama na kufuta jasho lake]: "Ahsonde soona." *[anawapa shilingi kumi yule mvulana na msichana waliosaidia. Anapofika hapo, mvulana sasa anaacha kujifanya mtalii.]*

MVULANA: *[akiwa na hasira kali]:* Nilimpa shilingi kumi kwenda kuvunja, hali huku nikiongea na Mwamerika mwingine. Lakini hakurudi. Nilimtafuta Nairobi yote, lakini akawa akijificha kila aliponiona. Nairobi ni mji mkubwa, siyo kama Nyeri ambao ni kama kijiji. Alinitoweka kabisa. Na halafu kukatokea msukosuko wa Anvil, na nikaletwa hapa. Leo kwa bahati nzuri nikamwona.

MWANAMKE: Kwa hivyo ukaonelea umpige? Na kweli ungemuua kwa sababu ya shilingi tano! Shilingi tano ulizopewa na mzungu?

MVULANA: Kuna wengine ambao wameuliwa kwa kiasi kidogo ya hicho.

MWANAMKE: Huna haya? *[anamtazama kwa jicho la kumkumbuka]:* Nimekutazama tangu ulipoanza kunihadithia kisa chako, na sasa najua kwa yakini kuwa nimewahi kukuona mahali fulani. Uliku wa kiongozi wa vijana waliokuwa doria wa watengenezaji wa pombe kule Mathare, na kuwajulisha Polisi watokeapo. Ni kweli?

MVULANA *[anamtazama mwanamke kama kwamba ni nabii]*: Umejuaje? Nawe ulikuwa Nairobi pia? Tuliuita Mathare, mji wa uhai na kifo.

MWANAMKE: *[mwanamke anatoa kicheko cha dharau]*: Njoo hapa. Nitakupa pesa ulizokuwa ukipigania kuzipata kutoka kwa msichana yule.

Anamfuata. Mwanamke anachukua kikapu chake, anaangalia ndani, halafu mara moja anaonekana amekumbuka anachotaka. Anaketi chini, halafu kutoka ndani ya rinda lake anatoa kifuko kidogo cha pesa. Anatazama juu na kumwona mvulana anamtazama. Lakini anachotazama hasa si pesa bali mkate.

MWANAMKE: Una njaa, sivyo?

MVULANA: Sijala chochote tangu jana.

MWANAMKE: Haya. Chukua hii noti ya shilingi ishirini. Nenda ukajinunulie chochote ule. Na uniletee baki yangu papa hapa nilipo.

MVULANA: *[anachukua pesa huku akiwa haamini]*. Ahsante sana mama. Hakika nashukuru sana. *[anaondoka mbio jukwaani.]*

MWANAMKE: Mungu wangu! Mambo ni yale yale. Kila mahali. Mombasa, Nakuru, Kisumu, Eldoret. Hadithi ile ile.
Watu wetu wanauana . . . na yote kwa sababu ya makombo wanayotupiwa na walowezi wanyonyaji. Chakula chetu chenyewe ambacho kimeliwa, na sisi wenyewe tunatupiwa makombo katika nchi yetu wenyewe, ambako inafaa sisi tupate kile kinono. Tunanunua kuni kutoka kwenye misitu yetu wenyewe, tunatoka jasho katika ardhi yetu wenyewe kwa manufaa ya wadhalimu wetu. Mafundisho ya Kimathi yanatuambia: unganeni, mmuondoe adui, na msimamie utajiri wenu wenyewe na kufurahia matunda ya jasho lenu. Na ni kwa sababu hii adui amemtia nguvuni. *[mvulana anaingia huku akila maandazi kwa hamu kubwa.]*

MVULANA: Baki yako ni hii. Nakushukuru. *[anasimama hapo akiwa hajui la kufanya.]*

MWANAMKE: Keti ule pole pole. Hakuna mtu atakayekichukua chakula chako. Kama ningekuwa mama yako ningekufanya uoshe mikono yako michafu, ushone nguo zako, uzifue na kukufunza namna ya kula vizuri.

MVULANA: Sina mama.

MWANAMKE: Huna!

MVULANA: Ndiyo. Alikufa wakati alipokuwa akinizaa.

MWANAMKE: Na baba yako je?

MVULANA: Baba alifukuzwa kutoka kwenye ardhi ya ukoo hapa Nyeri na mmoja wa jamaa zake aliyekuwa mkalimani wa mahakama. Mtu huyo sasa ni chifu mkuu wa serikali, na ana ardhi kubwa. *[bila mzaha]:* Lakini sitasahau siku wafuasi wa Kimathi walipochoma makao yake ya kupigana na Wazalendo. Makao hayo yalikuwa makaburi ya wananchi.

MWANAMKE: Je, wafikiri simjui mtu unayemzungumzia?

MVULANA: H'm. Mtu huyo alikuwa hodari sana katika kesi za mahakamani na alikuwa akiwahonga sana mahakimu. Mimi na baba tulikwenda Nairobi. Baba akapata kazi katika kampuni ya wafanyi biashara wa mbao, akakodisha chumba kidogo na kupata mshahara mdogo kila mwezi. Wakati huo nilikuwa sijui lolote. Nilikuwa nikimwibia kile kidogo alichopata kututosheleza yeye na mimi. Lengo lake lilikuwa kupata pesa za kutosha halafu kurudi Nyeri na kununua ardhi. Lakini hakufanikiwa katika ndoto yake. Mashine ilimkata mkono wake wa kulia, na akafa kwa kutoka damu nyingi. Matajiri wake hawakujisumbua kumsaidia. Nikafukuzwa kutoka chumba alichokuwa amepangisha.

MWANAMKE: Ulipata taabu kubwa, kweli!

MVULANA: Aaaa! Nairobi! Nimepambana na majibwa na mapaka katika kung'ang'ania makombo katika mapipa ya taka. Na nakumbuka mtambo wa kuoka mikate. Ulikuwa mali ya Mhindi. Mara kwa mara alitupa mikate iliyooza. Sote tuliipigania— Shimo hili ni langu, pipa hili ni langu. Paka, mbwa, wavulana kwa wasichana. Lakini tulijifunza namna ya kuishi na tukapevuka kabla ya wakati wetu kufika.

MWANAMKE *[anafikiri kwa makini]:* Hata mimi pia nimeishi mjini. Nafahamu maisha uliyoyaeleza. Kupigana . . . kulewa . . . kupigana . . . kulewa . . . kangari, karubu, busaa, chang'aa . . . Bonde la Mathare . . . Pumwani . . . hayo na zaidi. Nilikuwa mwanamke mwovu . . . niliishi maisha ya uovu . . . mpaka nili-

popata mwito.

MVULANA: Mwito? Wa Kristo?

MWANAMKE: *[anacheka]:* La. *[anabadili hali]:* Mwito wa watu wetu. Watu walioteswa, waliojeruhiwa, waliotukanwa, wanaonyanyaswa, mamilioni ya Wakenya wanaomfanyia kazi adui kwa manufaa yake.

MVULANA: Sielewi.

MWANAMKE: *[bila kusubiri]:* Na eti unajiita mwanamume! Ni kitu gani hukielewi? Mambo ninayokwambia yaonekana waziwazi kila mahali. *[ananyamaza kidogo]:* Siku utakapoelewa kwa nini baba yako alikufa; siku utakapojiuliza: "Nitafanyaje mwingine asife katika hali duni kama hiyo?" Siku hiyo mwanangu utakuwa umekuwa mtu mzima. Kwa sasa uko kama mnyama, na yule msichana alikuwa na haki ya kukuita hayawani.

Hebu. Chukua hizi shilingi kumi na tano, na usijaribu tena kumpiga msichana yule. *[anajifanya kama kwamba anaondoka.]*

MVULANA: Lakini . . . tafadhali . . . usiende bado . . . nataka kukuuliza jambo fulani.

MWANAMKE: Haraka. Nina kazi nyingi inayoningojea.

MVULANA: Sasa hivi, dakika chache zilizopita, ulinipa shilingi ishirini.

MWANAMKE: Ndiyo.

MVULANA: Uliniambia nikuletee baki.

MWANAMKE: Ndiyo.

MVULANA: Kitu gani kilikufanya ufikiri kuwa ningeirudisha?

MWANAMKE: Kwani hukuwa ukimpiga msichana kwa kutokukuletea baki yako?

MVULANA: Lakini mama!

MWANAMKE: Sema nisikie!

MVULANA: Nataka kukuungamia. Nilitaka kukimbia nazo.

MWANAMKE: Kwa nini hukufanya hivyo?

MVULANA: Sijui. Lakini nilijiona narudi.

MWANAMKE: Nilijua. Nilijua kuwa ungerudi.

MVULANA: Lakini mama!

MWANAMKE: Sema tu!

MVULANA: Sijui nikushukuru namna gani kwa vile ulivyofanya leo. Lakini . . . lakini . . . kama naweza kufanya lolote, lolote unalotaka . . . kama kufagia nyumba yako, kulimia mimea yako, ama hata kukufulia nguo zako.

MWANAMKE: *[kwa hasira]:* Unataka kubadilisha mabwana sasa! Unataka kuwa na bwana mweusi badala ya mweupe! Huna mawazo mengine ila kuendelea kuwa mtumwa! Kama nisingekuwa na mambo muhimu ya kufanya, bila shaka ningekutandika sawasawa.

MVULANA: Siyo hivyo . . . Siogopi kazi . . . kazi yoyote!

MWANAMKE: *[karibu aondoke, lakini mara wazo linamjia. Anamtazama mvulana kwa makini, anatazama saa yake iliyo ndani ya mfuko wake, halafu anamtazama tena kijana]:* Ni kweli kwamba ungependa kufanya kazi? La, shughuli? Uko tayari kuwa mwanamume kamili?

MVULANA: *[kwa fahari kubwa]:* Ndiyo, niko tayari.

MWANAMKE: Tayari kwa kila kitu?

MVULANA: *[aonyesha kukasirika]:* Kwa nini unanionea shaka? Nipe kazi yoyote, mahali popote, nitaifanya.

MWANAMKE: Basi sikiza kwa makini. Dedan Kimathi ametiwa nguvuni.

MVULANA: Ndivyo wanavyosema watu. Lakini ni kweli wasemavyo?

MWANAMKE: Nini?

MVULANA: *[kwa kutaka kujua]:* Wanasema, wanasema . . . kuwa alikuwa akizungumza na Mungu.

MWANAMKE: Ndiyo, aliongea na Mungu aliye ndani yetu sisi tunaogandamizwa.

MVULANA: Wanasema . . . aliweza kutambaa kwa tumbo lake kwa maili kumi ama hata zaidi.

MWANAMKE: Ilibidi awe na nguvu kutuhudumia sisi sote wana Kenya.

MVULANA: Pia wanasema aliweza kujigeuza ndege, upepo, chochote kile?

MWANAMKE: Imani katika kupigania haki inaweza kufanya miujiza.

MVULANA: Wanasema kuwa mti aliokisalia chini yake ulianguka?

MWANAMKE: Kuna watu mwanangu waliojaliwa. Na ikiwa kutatokea chochote kwao, basi hata upepo, mvua na hata jua vinaweza kutoa ishara. Hata vifo vya mafisi vinaweza kutetemesha milima na kuanzisha milipuko ya volkeno zilizokuwa zimetulia kwa karne nyingi.

MVULANA: Labda walitia nguvuni kivuli chake, ama wasemaje?

MWANAMKE: Maneno yako yana busara mwanangu. Kimathi hakuwa pekee na hatakuwa pekee hata kidogo. Hakuna risasi inayoweza kumuua ikiwa wanawake wataendelea kuzaa watoto. *[kwa mkazo zaidi]:* Hata tupigwe risasi nyingi namna gani, ninachoamini ni kuwa siku moja ardhi itarudi mikononi mwa wenyewe.

[anasita]: Lakini sikiza kwa makini. Kuna udhuru ambao nataka uufanye. Kimathi atapelekwa mahakamani leo. Leo mchana. Unaweza kufanya jambo fulani kwa niaba yake?

MVULANA: Nitafanya kila niwezacho kutimiza udhuru huo.

MWANAMKE: Maneno ni rahisi kutamka. Lakini ni vitendo vinavyodhihirisha kuwa kweli u mwanamume.

MVULANA: Niko tayari.

MWANAMKE: Unajua mahakama ilipo hapa Nyeri?

MVULANA: Si mbali na jela ya rumande. Karibu na Baraza la Wananchi.

MWANAMKE: Barabara. Hapo, karibu na milango ya jela ama nje ya mahakama, utamkuta mtu akiuza machungwa. Utamtambua kwa sababu atakuwa amevaa shati jekundu. Utasikia akiimba: "Machungwa ni rahisi leo, Thandaraita-aaa." Mpe mkate huu.

MVULANA: *[akishangaa]:* Hii tu?

MWANAMKE: Mkate ni uhai!

MVULANA: Mkate kwa Dedan?

MWANAMKE: Lazima uwe mwangalifu sana. Unachobeba kina thamani ya uhai. Wasikia?

MVULANA: Lakini mkate. Mkate tu!

MWANAMKE: Ndiyo. Uulinde kwa nguvu zako zote. Nitakuwa nikikutazama. Nenda salama na uichunge kila hatua yako. *[anatoka nje.]*

MVULANA: Dedan Kimathi. Mkate. Kesi. Haiwezekani! Haiwezekani! *[linamjia wazo la ghafla]:* Mama! *[anamkimbilia lakini amechelewa]:* Oh, amekwenda sasa. Hakuniambia jina lake, ama mahali tutakapoonana.

Anasimama wima na huku anasikia sauti ya mnong'ono.

SAUTI YA MWANAMKE: Siku utakapojiuliza . . . nitafanyaje mwingine asife katika hali duni kama hiyo . . . siku hiyo mwanangu utakuwa umekuwa mtu mzima.
[anatoka.]

ONYESHO LA PILI

Barabara

Barabara nje ya mahakama. Umati mkubwa unaonekana. Mwanamke ambaye amejifanya mwanamume kwa kuvaa shati jekundu, anaonekana akiuza machungwa kutoka kikapuni.

MWUZAJI MATUNDA: Machungwa rahisi leo
Machungwa rahisi leo
Unapoelekea mbinguni
Utahitaji chungwa

Wapitaji wanashangazwa na sauti ya mwuzaji matunda kwa hivyo wanasimama kumtazama.
Kwanza wanaonekana Waafrika, halafu Wazungu. Mwuzaji matunda anatazama saa yake, na halafu ghafla anaufuata umati. Baadhi ya watu wamevutiwa na uuzaji wa mtu huyo.

MWUZAJI MATUNDA: Utamu . . . Gucamirwo-oo
Ukimeza, chozi lajimwaga!
Ni utamuuu . . . tam-tamuuuuu . . .
Kuheherwona gucamirwo.
[Sauti yake inafifia kundini.]

Mahakama

Onyesho linabadilika na kuwa ndani ya mahakama. Jukwaa lazima lipangwe kwa njia ambayo laweza kubadilishwa kuonyesha ndani.

Wanawake Wazungu waliovalia kama kwamba wanakwenda kwa maonyesho ya mitindo ya mavazi wanaingia wakifuatiwa na waume zao ambao mishipi yao imejaa bastola. Wazungu wote wanaketi upande mmoja. Waafrika wanaingia wakiwa wamevalia nguo za kutatukatatuka na viatu vilivyopasuka. Wanakaguliwa kwa makini na askari Mwafrika chini ya uangalizi wa Waitina.

Fimbo ama kitu chochote ambacho chaweza kutumiwa kama silaha kinatwaliwa. Wakati wote mahakama inapoendelea, Waafrika wanaonekana wenye chuki na hasira kwa maafisa wa kibeberu huku wakipendezwa na msimamo wa Kimathi. Karani wa mahakama anaonekana akiandikaandika mambo fulani, halafu anaweka karatasi kadhaa kwenye meza ya hakimu. Waafrika wameketi upande mwingine wa mahakama mbali na ule wa Wazungu kama kwamba kuna bonde kubwa kati yao. Kila mtu yuko kimya, lakini watu wachache wanasikika wakiongea kwa sauti ya chini, kutoka pande zote. Karani anawaamuru wanyamaze akiwa na lengo la kuwanyamazisha Waafrika. Lakini jinsi alivyosema haifahamiki aliwaamuru watu wa upande gani. Mmoja kati ya walowezi anajichomoza kundini na kuelekea jukwaani alipo karani na kumshika ukosi wa shati.

MLOWEZI: Unathubutuje?

KARANI: Samahani bwana! Nasikitika bwana!

Waafrika wanaonyesha wamekasirishwa na hatua hiyo na wanajitayarisha kuja mbele. Walowezi (Makaburu) wachache wanatoa bastola zao.

KARANI: Nilikuwa nikiwaambia wale, bwana . . . siyo nyinyi. Mungu mmoja sikuwaambia nyinyi.

Afisa mmoja mweupe wa Polisi anawajia kwa haraka.

AFISA WA POLISI: Rudisheni bastola zenu mara moja na mrudi kuketi

Kabaila aliyeanzisha zogo hilo na weupe wenzake wana-nung'unika juu ya "Waafrika walioelimika". Lakini mwisho wanarudi vitini mwao shingo upande. Karani anajaribu kure-kebisha ukosi wa shati lake, anakohoa kidogo na kuketi. Ghafla anasimama.

KARANI: Simameni, mahakama sasa inaanza shughuli zake.

Anaingia Shaw Henderson aliyevalia kama hakimu. Anaketi chini, na watu mahakamani wanaketi baada yake. Karani ana-mpa jalada la kesi, na hakimu analiangalia.

HAKIMU: Mleteni mshtakiwa.

Kila mtu kimya. Hakimu anajifanya kutojali, lakini naye pia mwisho anatazama kule anakotazama kila mtu. Dedan Kimathi analetwa akiwa amefungwa minyororo miguuni na mikononi. Analindwa na askari wenye silaha tayari kwa lolote. Anasuku-mwa kizimbani na Waitina ambaye anaandamana na Askari wa Kwanza na wa Pili.

Ni kimya kabisa.

HAKIMU: Dedan Kimathi bin Wachiuri, au kwa jina jingine Waziri Mkuu ama Jemadari, asiye na makao maalum, unashta-kiwa kwamba usiku wa Jumapili ya Tarehe 21 mwezi wa Oktoba, mwaka 1956, ukiwa Ihururu ama karibu na hapo, uli-patikana ukiwa umebeba bunduki ya aina ya *revolver*, bila leseni, kinyume cha Kifungu 89 cha Sheria za Nchi hii, jambo ambalo kulingania na hali ya hatari iliyopo nchini, ni kosa la jinai. Je, wakiri ama wakana mashataka hayo?

KIMATHI: Una uwezo gani wa kunihukumu mimi, wewe hakimu wa kibeberu?

HAKIMU: *[akichezea miwani yake, huku akingojea]*: Kimathi, nataka ukumbuke kuwa tuko katika mahakama ya sheria.

KIMATHI: Mahakama ya sheria za kibeberu.

HAKIMU: Nakufahamisha kwamba unakabiliwa na mashtaka ya ji-nai, ambayo adhabu yake ni kifo.

KIMATHI: Kifo . . . .

HAKIMU: Ndiyo, kifo. . . .

KIMATHI: Kwa hakimu mhalifu, katika mahakama halifu. Iliyoanzishwa na sheria za kihalifu, sheria za kugandamiza. Sina zaidi.

HAKIMU: Pengine huelewi. Pengine muda mrefu uliokaa msituni ume . . . nina maana kwamba . . . tuko hapa kukufanyia haki, kuona kwamba sheria inatekelezwa.

KIMATHI: Sitakubaliana na sheria ambayo hatukuhusika katika kuitunga.

HAKIMU: Sheria ni sheria. Kila jamii iliyostaarabika inahitaji utawala wa sheria. Haki ni haki.

KIMATHI: Sheria ya nani? Haki ya nani?

HAKIMU: Kuna sheria moja tu na haki moja.

KIMATHI: La! Sheria mbili na haki mbili.

Sheria moja na haki moja huwalinda wenye rasilimali, tajiri, wanyonyaji walowezi. Haki nyingine hunyamazisha masikini wenye njaa, watu wetu.

Waafrika wanashangilia. Wazungu wametuna kwa hasira.

HAKIMU: Siongei juu ya sheria za msitu wa Nyandarua.

KIMATHI: Msitu wa ukoloni na unyonyaji? Kwani huko ndiko utakapowakuta wanyonyaji wakubwa wakinyonya damu za wale wanaozalisha mali:

Sisi.
Tunaoendesha viwanda
Sisi
Tunaovumilia mateso
Tuliofanywa viwete
Tuliovunjwa migongo
Tutiririkwao na jasho la damu
Tunaotandikwa viboko
Tunaokufa kwa njaa
Tunaodunishwa
Tunaotemewa mate
Tunaotandikwa mijeledi
Lakini

Tunaokataa katakata kushindwa
Tukingojea siku mpya
Itakayoangaza Kenya nzima.

HAKIMU: Najua u mshairi, msemaji na mwanasiasa. Hakuna nchi ambayo haina sheria za kulinda rasilimali . . . maisha yetu . . . Ustaarabu . . . Ukristo . . . na utengamano.

[kabaila aliyemshika ukosi karani anapendezwa na usemi huo na kutamka "Hapo umesema" kabaila wengine wanaitikia kwa kuinamisha vichwa. Hakimu hasemi kitu.

KIMATHI: Nashutumu sheria na mahakama zenu. Zimewafanyia nini watu wetu?
Nini?
Zimewalinda wanyonyaji.
Zikawaidhinisha wauaji watu wetu; wametandikwa kwa kukataa kuchuma chai na kahawa yenu.
Wakatiwa gerezani
Walipokataa kuwa mayaya wa wàtoto wenu, ama maboi wa nyumba zenu.
Wakanyongwa kwa kukataa kukokota magari yenu.
Natambua sheria na mahakama moja: sheria na mahakama ya wale wanaopigana na unyonyaji,
Wale wanaogandamizwa walio tayari kusema,
Tunadai uhuru wetu.
Hiyo ndiyo sheria yetu
Tunaonyanyaswa,
Tunaodhulumiwa,
Tunaotukanwa,
Tunaodunishwa,
Tunaojeruhiwa!
Vita
Mapambano
Mabadiliko.

HAKIMU: Hakuna uhuru bila sheria na utengemano.

KIMATHI: Hakuna sheria na utengemano bila uhuru.
Mmefunga miguu yangu,
Mmefunga mikono yangu,

Mmefunga roho yangu,
Na tena mwapayuka, sheria na haki?
Sheria ya wananchi inaniambia:
Nifungueni mikono yangu
Nifungueni miguu yangu
Nifungueni roho yangu!

Waafrika wampigia makofi kwa shangwe. Wazungu waghadhabika. Walinzi wanajiweka tayari.

HAKIMU: Kimya kortini! *[anasimama]:* Kesi imeahirishwa. Mshtakiwa atawekwa rumande hadi kesho kesi itakapoendelea.

Kila mtu anasimama. Hakimu anatoka. Mara hakimu anapotoweka kabaila mwenye hasira anamwendea mfungwa huku akiapa. Kabaila wengine wako tayari kwa vyovyote. Walinzi wanamkamata Kimathi na kuanza kumtoa mahakamani kwa haraka.

MLOWEZI: *[akimwelekezea bastola yake Kimathi huku akipayuka kwa hasira]:* Mwanaharamu Mau Mau. Na sheria ya Mwingereza imeweza kuvumilia wazimu wa mtu huyu!
[akiwapigia kelele walinzi]: Askari, mwacheni ama nitawapiga risasi pamoja na komunisti hilo la mwituni!
[akipiga makelele kwa sauti ya juu zaidi]: Field Marshall/Waziri Mkuu. Sokwe mweusi. Sikiza wewe ngiri, leo ndio mwisho wako. Nitakufunza haki.
[anajaribu kutoka kupitia mlango aliopitia Kimathi, lakini ghafla anageuka na kuwatazama watu katika mahakama]:
Nilikuwa na maelfu ya ng'ombe na kondoo. Wako wapi sasa?
Nilikuwa na maelfu ya ekari za mahindi na ngano, ziko wapi sasa?
Nilikuwa na mke na binti.
Wako wapi sasa?
Wameuawa, wamechomwa moto. Wamekatwakatwa na huyu mwenda wazimu pamoja na majambazi wenzake.
Ni yupi mwenye rasilimali ambaye yuko raha mstarehe siku hizi?

Bia na wiski hazinyweki.
Hebu nione mimi. Si mtu mvivu.
Hata kama siko kama Delamere na Grogan
Lakini si mvivu
Nilifika hapa kama askari
Askari wa kawaida
Nilipambana na mikopo ya mabenki, ofisi ya kikoloni, vyote vilinilemea.
[anaelekeza bastola yake upande wa Waafrika]:
Mwafikiri lilikuwa jambo rahisi?
Na nilipokuwa tayari kufurahia matunda ya jasho langu
Mlianza uharamia
Nilikuwa na uhusiano mzuri na maboi wangu
Pia nao walifurahia kufanya kazi shambani mwangu
Niliwapa posho, nikawajengea shule, zahanati . . . niliwapa kila walichohitaji.
Walinipenda
Ndiyo, huko Olkalau walikuwa wakisifu shamba langu:
Halafu huyu shetani, Jemadari, akaja kuwapotosha akili zao na fujo zake, na kusababisha vifo vya karani wa maziwa, karani wa viapo!
Sasa basi, nanyi mtakufa.

[Makelele ya hofu na fujo wakati mlowezi anapotisha kuwaua Waafrika. Kwa kuwa amesimama mlangoni, njia ya kujisalimisha ni kupitia madirishani.]

MWANAMKE MZUNGU MZEE: Dick, usifanye hivyo!
[akiwa ametishika]: Mpokonyeni hiyo bastola haraka. Yote haya yametokana na hawa hayawani.
[Waafrika wamekasirishwa na usemi huo.]
AFISA MZUNGU: *[ameandamana na askari wa KAR wa Kiafrika na kumwendea mlowezi]:* Bwana Windhoek, rudisha bastola yako. Sheria itatekeleza haki ipasavyo.
MLOWEZI: *[akisita]:* Sheria gani?
Hiyo ni dhihaka kubwa.
Tena hakimu ameweza kuvumilia!

La hasha. Mimi sitavumilia upuzi huo
Bastola hii itakuwa hakimu wangu!
[akipambana na afisa mzungu huku akitweta kama mwenda wazimu]:
Jemadari, Bwana Ded . . . Ded . . . Kimathi. Nitakuua kwa mkono wangu.
[Wakati wa mapambano hayo risasi inalipuka. Mwisho mlowezi anazidiwa nguvu na kutolewa nje. Askari wanawatoa watu kutoka mahakamani.]

Barabara

MWUZAJI MATUNDA (MWANAMKE): Machungwa rahisi leo
Machungwa rahisi leo
Thandaraita-i
Kuheherwo na gucamirwo
Thandaraita – aaaaaaa!
[Mwuzaji matunda anajiingiza katika kundi la watu wanaotoka mahakamani. Watu hawamjali lakini yeye anaendelea kuuza matunda yake. Watu wanatoweka na mwuzaji matunda anabaki jukwaani. Anatazama hapa na pale kama kwamba alikuwa akitazamia kumwona mtu fulani]:
Thandaraita-i
Thandaraita – aaaaaaa
Kuheherwo
Kuheherwo na gucamirwo
Tamu — uuuuuu!
Ukimeza chozi lajimwaga
Thandaraita-i
Thandaraita – aaaaaaa!
Ukiwa unaelekea mbinguni
Utahitaji chungwa.

Anatoka. Anaingia mvulana akibeba mkate aliopewa na mwanamke.

MVULANA: Aliniambia angekuwa hapa, lakini sijamwona mwuzaji matunda ama mwuzaji machungwa yeyote. Yule mwanamke!

Kwa nini hakuweza kuubeba mkate mwenyewe? Aliogopa. Aliogopa kabisa. Kwa nini basi alinitazamia kuhatarisha maisha yangu kwa kumpelekea mkate Kimathi? Tena nimesikia kuwa Kimathi hali mikate.

Na je, kama hawakumtia nguvuni Kimathi bali kivuli chake? *[anafanya kama anataka kuondoka]:* Lakini nitamwona wapi mwanamke huyo? Sasa najua. Hakutaka nimpelekee mkate huu mtu yeyote. Alitaka tu kunijaribu, aone kama ningeula. *[anavunja kipande]:* Lakini alisema angenitazama wakati wote. *[anajaribu kukirudisha kipande hicho. Katika kufanya hivyo, hamwoni msichana akiingia. Msichana anamwona na kusita. Anajaribu kumpita. Mvulana amwonapo anaachilia mbali anachofanya.]*

MVULANA: Wewe. Pesa zangu!

MSICHANA: Sina pesa.

MVULANA: Nitakuonyesha.

[anajaribu kumzuia msichana, lakini anaezekwa kofi. Msichana anakimbia. Mvulana anaokota mkate na kumfuata.]

Shawishi la I

Sehemu zote nne za kumshawishi Kimathi zinafanywa ndani ya chumba alimofungiwa. Lakini chumba hicho kipangwe kama mahakama. Kimathi anaketi pembeni akiwa amefungwa minyororo miguuni. Pia analindwa kwa ulinzi mkali. Henderson anapoingia, Kimathi anaonekana ameegemea ukuta. Henderson anaingia kwa utaratibu huku akimsikiza Kimathi anayeongea peke yake.

KIMATHI: Ndoto. Njozi.
Karuna-ini
Ihururu
Muthunduri
Mabonde ya miwa ya wakati wa ujana wangu
Matuta ya kijani ya wakati wa ujana wangu.
Kijito cha Ndi-ini
Nilipozoea kuoga

Kujitumbukiza katika maji yake baridi!
Sasa ndoto hizo zanijia
Sehemu hizo na njia nilizopitia msituni hapo mwanzoni.
[Sasa anahutubia mtu ambaye haonekani . . . mama yake mwenda wazimu.]
Masikini mama yangu . . . La . . . usilie.
Sikukosea nilipochagua njia ya ukombozi.
Ningelikutazamaje machoni mwako?
Nisamehe. Nisamehe.
Mapenzi yako kwangu
Yamekupa wazimu!
Lakini ushindi utakuwa wetu
Mama yetu, sisi watoto wako.

HENDERSON: Bwana Dedan. Jemadari. Majinamizi ya kukiri?

KIMATHI: Wewe ni nani?

HENDERSON: Bwana Shaw Henderson! Watu wako wote wananifahamu. Mimi ni rafiki.

KIMATHI: Shaw Henderson! Rafiki na muuwaji wa Waafrika, ugh!

HENDERSON: Shida yako, wewe Dedan, ni kwamba una shaka kila wakati. Hebu nione, nimekuja kwa amani wala sikubeba silaha yoyote.

KIMATHI: *[kwa hasira]:* La, hukubeba silaha, lakini umebeba maneno. Hotuba. Ahadi za kuvutia. Kwa hivyo usijisumbue bure.

HENDERSON: Sikiliza Dedan. Watu wako wananiamini. Wamenituma niongee nawe ili uweze kuona mwangaza.

KIMATHI: Unanihadaa! Watu gani?
Waaminifu? Walinzi wenu? Wasaliti? Hao ni watu wako *[anatoa kicheko cha dharau]:* Lenana, Wang'ombe, Karuri Gakure, Njiri, Waruhiu, Luka Kinyanjui, Mumia . . . Sikiliza Bwana Shaw Henderson — rafiki wa Waafrika — huwezi kunihadaa hata ujifanye namna gani. Hata ulipokuwa ukija nilikuona ndotoni. Watumwa wote uliowahadaa hapo mbeleni. Mshikaji watumwa we!

HENDERSON: Unaota tena? Wakumbuka barua uliyowahi kumwandikia kakako Wambararia?

KIMATHI: Kwa nini unichokeshe masikio yangu na majina ya wasaliti?

HENDERSON: Hujapata kumpenda. sivyo? Yeye ni mmoja wa wale wanaotusaidia.

KIMATHI: Alijitolea kwa sababu ya tumbo lake mwenyewe.

HENDERSON: Uliogopa uongozi wake. Uliogopa uongozi wa kila mtu . . . Jemadari China. Stanley Mathenge.

KIMATHI: Woga? Sijaogopa uongozi wa mtu yeyote. Nimekuwa nikipigania watu wasisaliti mapambano yetu kwa manufaa yao binafsi.

HENDERSON: *[akimtania]:* Hiyo ndiyo sababu ya wewe kuendelea kuishi.

KIMATHI: Una maana gani kwa usemi huo? Beberu wa Kiingereza! Wewe u nani wa kutoa idhini ya mtu aendelee kuishi ama asiendelee kuishi?

HENDERSON: Sikiza, Kimathi, nimekuja kwa shughuli maalum.

KIMATHI: Mashauri, mikataba, mapatano. Mmeangamiza mataifa mangapi halafu mkadai eti kulingana na mkataba huu na ule mataifa hayo yalitoa ardhi na maisha ya watu wao.

HENDERSON: Sikiliza, Dedan. Mimi ni askari.

Ni kweli kwamba wakati fulani ninakuwa kachero, mwindaji wa watu, lakini moyoni mwangu mimi ni askari. Wito wa askari ni kusema jambo mara moja bila kusema hili ama lile mwanzo. Fahamu kuwa mimi si mshairi kama wewe. Kesho itakubidi ukiri makosa yako mahakamani.

KIMATHI: Nikiri? Makosa? Nikiri makosa.

HENDERSON: Usinitazame kwa macho yako mekundu.

KIMATHI: Wafikiri nimehadaika?

HENDERSON: Lini?

KIMATHI: Leo. Katika mahakama yako ya kuchekesha.

HENDERSON: Una maana gani?

KIMATHI: Lazima nikuambie kuwa ulivutia katika nguo zao za uhakimu.

HENDERSON: Toleo langu si la dhihaka.

KIMATHI: Endelea. Niambie toleo lako, ama mtego wako.

HENDERSON: Nimekwisha kukueleza kuwa una hamaki kubwa. Toleo langu halina mtego wowote. Nakuhakikishia kama mwungana wa Kiingereza. Ukikiri makosa yako, hatutakunyonga.

KIMATHI: Ninyi? Msininyonge? Ni nini msingi wa huruma hiyo? Si kila mmoja wenu anapigania kupata kichwa changu?

HENDERSON: Tunataka vita hivi vikome. Stanley Mathenge bado hajapatikana. Kuungama kwako na ushirikiano wako kwa jumla unaweza kuwafanya wajitolee.

KIMATHI: Na ungepata tuzo kubwa kwa jambo hilo . . . nishani ya George! Nishani! Nishani! Ni lazima uangamize mataifa kwa sababu ya kupata nishani?

HENDERSON: Sikiza bwana, wewe na mimi hatuna haja ya kujifanya. Mataifa yanaishi kulingana na nguvu zao na heshima zao. Ulitisha matakwa yetu, nasi ilikuwa haina budi kuyapigania na kuyashinda. Ni kwa manufaa yako pia kwamba tunamaliza vita hivi vibaya.

KIMATHI: Hayo ni maneno matamu ya kuvutia yanayotoka kinywani mwa nyoka. Wafikiri naweza kuwa mpumbavu wa kuyatia maanani?

HENDERSON: Hata wenzako wamesema nayo unayotamka sasa, China, Gati, Hungu, Gaceru na hata Wambararia kaka yako mwenyewe! Wote wanaotusaidia. Kwanza hawakuamini kuwa ningetimiza ahadi yangu kwao lakini sasa tazama, tumehifadhi maisha yao.

KIMATHI: H'm. Una maana kuwa mmeyateka maisha yao!

HENDERSON: Kwa nini ubatilishe usemi wangu namna hiyo, Dedan? Hebu sikiza, pengine hutaniamini lakini nakuhakikishia kuwa nakuthamini sana. Hukumbuki ule wakati wa ujana wetu, tulipokuwa tukicheza sote kwenye mitelemko ya mlima Kenya? Unakumbuka siku ile tulipocheza mchezo wa mpanda farasi? Tulianguka. *[anacheka.]*

KIMATHI: Una maana kuwa nilikuangusha! Nawe ukaenda kwa mamako huku ukilia.

HENDERSON: Lazima ujue kuwa ulinifanyia vibaya!

KIMATHI: Ndiyo. Kwa sababu ulinitaka mimi niwe farasi na wewe uwe mpandaji.

HENDERSON: Lakini rafiki yangu, si lazima kuwe na farasi na mpanda farasi? Sasa maana ya mchezo wa mpanda farasi ingeeleweka namna gani?

KIMATHI: Ni lazima pawe na farasi na mpanda farasi, sivyo? Basi ni heri niwe kama punda wa Balaam. *[anatoa kicheko cha dharau]:* Ndiyo, punda aliyemkataa mpandaji wake. *[anasita]:* Mwindwa akijua kwa yakini kuwinda windo lake, basi mchezo wa uwindaji utamalizika.

HENDERSON: Huwezi kusahau habari za msituni kwa muda mrefu, sivyo? Mauaji haya yana uzuri gani? Watu wako, Dedan, ndio wanaomalizika.

KIMATHI: Ndiyo tumepata hasara kwa sababu ya serikali ya Kiingereza. Lakini hizi ni nyakati nyingine kabisa. Hivi ni vita vya aina nyingine. Tumeuwawa kwa niaba yenu. Tumepigana katika vita kwa niaba yenu. Tumepambana na Wajerumani, Waitaliano, Wajapan. Lakini sasa tunakufa kwa ajili ya ardhi yetu, kwa ajili ya uhuru wetu, hadi mtakapojiondosha.

HENDERSON: Umeanza ndoto zako za mchana tena.

KIMATHI: Ndiyo. Na nitaendelea kuota hadi ndoto zangu zitakapodhihirika na watu wetu kuwa huru.

HENDERSON: *[akiwa amevunjika moyo katika juhudi zake za kumshawishi Kimathi]:* Lazima niseme kweli kuwa nakuthamini kwa nguvu zako, na fahari yako. Nawapenda watu wako na nchi yako. Hiyo ndiyo sababu iliyonifanya kuja kwako kama rafiki ili nijaribu kukusha—

KIMATHI: *[bila kusubiri amalize]:* Kimathi wa Wachiuri hataweza kamwe kusaliti mapambano ya wananchi. Asilani!

HENDERSON: Hebu nisikize, kwa manufaa yako mwenyewe. *[Kimathi anageuka, lakini Henderson aendelea na hotuba yake]:* Ninafahamu habari zote za ukoloni. Baba yangu alikuja kutoka Scotland. . . . Hata sisi tumetawaliwa na Waingereza. Ni lazima niseme wazi, Mfalme Jones. Ni wazi kwamba hangefurahia sana maisha ya Scotland. Huko kitu kikubwa ni jini la majini ambalo watu wengi hutamani kuliona bali ni wachache wapatao wasaa wa kuliona. Lakini hapa mambo yalikuwa mazuri sana. Mikopo, vilabu, Gymkhana, kuwinda, hasa mawindo ya Limuru ambayo kila mtu wa jamii ya Kifalme aliyatazamia sana. Kweli, hotuba yako uliyoitoa mahakamani ilikuwa nzuri. Ulisema ukweli kabisa. Lakini kwa kuwa nilikuwa hakimu niliku-

wa sina budi kutopendelea upande wowote. Mapambano. Sisi pia tuna haki ya kufanya mapambano, kuvumilia, kuhifadhi. Mambo ya kisasa, Ukristo na ustaraabu. Mimi pia ni Mkenya kwa haki na kwa nguvu zetu. Haki ni nguvu, amini usiamini. Nilikulia Nyeri. Ninachopigania ni haki yangu tu. Lakini jasho na fikira zimetua katika mapambano haya. Dedan Kimathi, ni lazima uungame makosa yako. Maisha ni muhimu kuliko fahari. Uliapa kwamba hungewèza kutiwa nguvuni na Mzungu yeyote. Lakini sasa uko ndani, ukingojea kunyongwa ama kusamehewa. Kiri, ungama, ungama makosa yako. Ukikiri makosa yako tutakuhifadhia maisha yako. Ni lazima tumalize vita hivi. Kiri makosa yako nawe utaruhusiwa uendelee kuishi.

KIMATHI: *[amekasirika, anamshika shingo Henderson]:*

Maisha. Maisha yangu. Unataka kutoa maisha yangu kwa kusalimisha yako.

Wewe ni nani, beberu mla watu, kunihakikishia uhai wangu?

Maisha yangu ni watu wangu,

Wanaopambana

Wanaopigana

Sio kama wewe unayetaka kuendeleza

Utumwa

Udhalimu

Unyonyaji

Lakini

Wanaopigana kumaliza utumwa, unyonyaji na ukupe.

Toka nje, panya we!

Rudi kwa mabwana zako waliokutuma na uwaambie: Kimathi hataisaliti Kenya kwa Waingereza ama kwa wanyonyaji wengine wa kigeni, sasa na hata wakati ujao.

HENDERSON: Mlinzi! Mlinzi!

[milango inafunguliwa na walinzi wanaingia wakiwa na bastola tayari. Kimathi anamwachilia Henderson]:

HENDERSON: *[akihema]:* Nitakuwahi tu kwa vyovyote. Naapa kuwa utakiona cha mtema kuni. Mimi, Shaw Henderson, utanitambua. Najua akili za Mwafrika. Utanitambua tu.

[anatoka nje.]

Shawishi la II

KIMATHI Aniokoe maisha yangu! Tangu lini mkoloni akaniokoa maisha yangu? Hebu sikizeni upuzi huo watu wangu! Mimi Kimathi wa nasaba ya Iregi.
Niliyebarikiwa na nyanya yangu kipofu, mkulima!
Alinipa nguvu zake, nguvu za watu wetu.
Niliihisi imani yake, nguvu zake zikiniingia mifupani mwangu.
Moto na mwangaza!
Aniokoe maisha yangu?
Labda maisha ya mtu mwingine!
Ni kweli kwamba siku zote nimetaka ngoma za watu wetu.

IGIZO: *[Makundi mbalimbali ya wacheza ngoma za kitamaduni yanatokeza jukwaani moja baada ya jingine. Kila kundi lina-lomaliza kucheza linajipanga kando ya jukwaa.]*

KIMATHI: Walikuwa wakicheza ngoma hizi
Kabla ya mkoloni kuingia nchini
Walizicheza wakati wa tohara, matanga, arusi
. . . Halafu mara mkoloni alipoingia, watu wetu wakaanza kuigiza michezo yao.

Gavana wa kikoloni anawasili. Ngoma ya kitamaduni inaanza kupungua. Wachezaji wanaingiwa na hofu. Wanacheza kwa hofu na halafu wanatoweka wakifuatwa na Mkuu huyo wa kikoloni.

KIMATHI: Jamani watu wangu!
Tunawezaje kuimba na kucheza namna hii ugenini?
Tunawezaje kuimba na kucheza namna hii,
Wakati maji kila mahali yako machungu?
Tunawezaje kucheza nyimbo za kudunisha na kutia hofu?
Haya yalikuwa . . . la, haya ndiyo maswali.
Katika kupambana nayo,
Niliwaongoza vijana
Tulikutana kutoka kila pembe ya Karuna-ini.
Tulijiita Gichamu

Tukatunga nyimbo mpya za kusifu mapambano yetu kujitayarisha kwa vita.

IGIZO: *[Wachezaji wanarudi wakiimba na kucheza wimbo wa mapambano ya uhuru.]*

KIMATHI: Tulisimama juu ya kilima cha Githuri
Upande wa kushoto ulikuwa msitu wa Nyandarua
Upande wa kulia ulikuwa mlima Kenya.
Na mbele yetu,
Zilikuwa ardhi zilizoibwa kutoka kwetu.
Ardhi zilizofika hadi kupita Nanyuki na Naro Moru, Nyanda za Nyeri tulizoibiwa
Tukajiuliza wenyewe
Ni mpaka lini
Sisi vijana wa Gichamu na Karuna-ini
Vijana wa nasaba ya Iregi
Tutaendelea kuwaacha watu wetu
Waendelee kuwa watumwa wa njaa, magonjwa na huzuni.
Katika ardhi yetu wenyewe
Na huku wageni wanaendelea kula
Na kukoroma vitandani wakiwa wameshiba?

Unaingia ujumbe wa wenye benki . . . au ujumbe wa wafanyi biashara. Mzungu katika ujumbe huo amevaa kama mabepari wa kutoka Ulaya. Mtu wa pili ni Mhindi na wa tatu ni Mwafrika ambaye haongei lolote bali anaitikia kwa kuinamisha kichwa chake.

MWENYE BENKI: Umesema kweli, Dedan. Njaa, magonjwa na kutojua kusoma na kuandika ndio hasa maadui wa watu wako.

KIMATHI: Wewe ni nani?

MWENYE BENKI: Wakati ni pesa. Mimi ama sisi ni wawakilishi wa mabenki, kampuni za bima na viwanda. Unaweza ukatuita wawakilishi wa jamii ya wafanyi biashara. Unajua Dedan, vita hivi vinarudisha maendeleo nyuma. Pesa ambayo ni ufunguo wa maendeleo sasa haiji.

KIMATHI: Maendeleo! Pesa. Pesa ni maendeleo?

MWENYE BENKI: Sikulaumu. Pengine hufahamu vizuri habari za uchumi na historia. Nilikuwa hapa hata kabla hujazaliwa. Standard Bank, National and Grindlays Bank, Barclays. Mimi ni mjenzi wa Kenya ya leo. Ni nani waliotoa pesa za ujenzi wa reli?

IGIZO: *[Makuli na Waswahili wanaonekana wakijenga reli. Wanafukuzwa na mashujaa wa Nandi wakiongozwa na Koitalel.]*

MWENYE BENKI: Waona? Hao ni watu wako! Juhudi zao za miaka kumi kidogo zingezorotesha maendeleo. Lakini baada ya ujenzi huo kukamilika, tazama matokeo yake: Makabaila. Delamere. Wawindaji, Askari wa kukodiwa. Sisi ndio tuliotoa pesa. Sasa unaweza kukubaliana nami kwamba waliibadilisha nchi hii. Sasa kuna miji ya kisasa kabisa. Mombasa, Nairobi, Nakuru, Eldoret, Kitale, Kisumu, na barabara za kisasa vilevile.

KIMATHI: Sema lililokuleta. Wataka nini? Ugomvi wangu sio na mabenki?

MWENYE BENKI: Ha! Ha! Ha! U mtu mwenye busara Dedan. La, hakuna haja ya kupigana na mabenki. Sisi ndio rafiki zako hasa. Kwanza tulikuwa na wasiwasi juu ya serikali ya Kiafrika. Tulidhani kuwa ingekuwa tisho kwa mali zetu, lakini tumepata hakikisho kutokana na serikali za Kiafrika za Ghana, Nigeria, Liberia na hata serikali ya India.

MHINDI: Maneno ote hii sava sava, Dedan. Katika Idia, sisi iko goument na uhuru. Iko uhuru ya kupanya biasara. Hii hapa iko rapiki yetu. Haweji bagua. Yeye iko vacha ninyi panya mambo ya tamaduni yenu. Ninyi weja omba Budha, Confucius au miti, weja omba mawe, waa sari . . . tamaduni yenu . . . nyimbo . . . machezo . . . ote hii majuri tu . . . maradi . . . sisi tengeneja peja . . . rapiki . . . rapiki.

KIMATHI: *[akiwa na hamu kubwa]:* Baadhi ya watu wetu walipitia India walipokuwa wanatoka Burma. Walipofika hapa walisema huko Calcutta, Delhi na Bombay waliwaona watu wenye njaa, waombaji . . . wanawake wanaojiuza kwa rupia moja . . . Je, wamesema hawataki umasikini sasa?

MHINDI: Sisi iko jaribu kodogo kodogo. Lakini, sisi iko dini yetu, bendera yetu, vimbo yetu ya taipa. Na sasa iko hata bapari ya benki Muindi . . . Ha! Ha!

MWENYE BENKI: Sikiliza. Sasa tuko tayari kuvumilia serikali ya Kiafrika, kwa kushirikiana nayo tu. . . .

KIMATHI: Hivyo tu?

MWENYE BENKI: Ungama. Tubu. Kiri makosa yako. Shirikiana na serikali kama wenzako walivyofanya. Waambie watu wako watoke msituni. Tunataka amani. Hakuwezi kuwa na maendeleo yoyote bila ya kuwa na amani. Tunaweza kujenga mahoteli makubwa ya hali ya juu . . . sehemu za watalii . . . Vilabu vya Usiku, Makasino, Barabara za Lami, viwanda vya kusafishia mafuta na mabomba ya kuyasafirishia kutoka kiwandani . . . Halafu utawaona watalii wakimiminika kutoka kila mahali, Amerika, Ujerumani, Ufaransa, Uswisi, Ujapani. Halafu rafiki yangu, rasilimali zitazidi na zitaimarisha maendeleo, ufanisi na kuleta raha.

KIMATHI: Na watu wangu je?

MWENYE BENKI: Watu wako ni akina nani?

KIMATHI: Wale wanaonyanyaswa . . . wote wale ambao nguvu zao zimebadilisha nchi hii.

Nchi hii imejengwa kwa jasho letu. Watu wetu watakuwa na wajibu gani katika mpango wako wa kushirikiana kwa ajili ya ufanisi?

MWENYE BENKI: Wapagazi ni lazima waweko. Wako kila mahali, hata Amerika, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Uswisi, Sweden na Ujapan. Kuna watumishi na matajiri . . . wauzaji wa nguvu zao na wanunuzi wa nguvu hizo.

Mabwana na watwana.

MHINDI: Hii maneno iko barabar. Hata dani dini etu tukupu, iko mabana na boi iko tu . . . Brahimin na ingine hapana kamata kwa makono.

KIMATHI: Dini ya utumwa! Ni kama ukoloni unaomfanya yule anayetawaliwa atoke jasho la damu na hali ni beberu atakayenufaika.

MWENYE BENKI: Ubaguzi wa rangi? La. Jambo hilo liliwezekana

katika miaka ya 1930. Lakini katika wakati huu ambapo tunazidi kuwapata Waafrika walioelimika *[anamwota Mwaafrika ambaye anainamisha kichwa kwa kuitikia]:* sasa hakuna haja ya ubaguzi wa rangi. Tumekuwa watu wa busara sana.

MHINDI: Barabar che.

KIMATHI: Pesa . . . Niwasaliti watu wangu? ASILANI.

MWENYE BENKI: Kama nilivyosema: Wakati ni pesa. Fikiria jambo hilo.

KIMATHI: *[akimwota mfanyi biashara Mwaafrika]:* Judasi! *Wanatoka.*

Barabara

Anaingia msichana akitembea polepole huku akifikiria sana.

MSICHANA: Nimechoka . . . nimechoka kukimbia. Maisha yangu yote nimekuwa mbioni tu.

Wanaume kunisumbua tu kila nifikapo. Nilikuwa binti wa heshima katika jamaa ya Kikristo. Tulikuwa katika sehemu ya ardhi iliyokuwa imekaliwa na Wazungu. Katika nyumba yetu mlikuwa na ilani: KRISTO NDIYE MKUU WA NYUMBA HII, MGENI ASIYEONEKANA KATIKA KILA MLO NA MSIKILIZAJI ASIYESIKIKA KATIKA KILA MAZUNGUMZO. Nilikimbia shuleni kwa sababu mkuu wa shule alikuwa daima ananiandama kutaka kunifanyia mabaya. Kila wakati alikuwa akiniambia, "Baki nyuma. Nichukulie kuni hadi nyumbani kwangu. Chukua chokaa hizi uzipeleke ofisini mwangu." Halafu angenifuata nyuma, na kile alichotaka ni kunigusa matiti. Kwa hivyo nikaacha shule. Nilitaka kukaa nyumbani nijifunze kushona ama mambo mengine ya manufaa, lakini jambo hilo halikumpendeza babangu. Aliniita mzembe na akanipeleka katika shamba la katili kabaila Jones kuchuma majani ya chai. Ukatili wake ulidhihirika wakati alipotutukana na kutuadhibu! Ilinibidi kutoroka kutoka nyumbani na kazini kwa katili Jones. . . na nilipofika mjini Nairobi nilianza kuandamwa na wavulana. Kila wakati wakinibughudhi na sikuwa na moyo wa kuvumilia

kufa kwa njaa. Nilipoteza ubikira wangu nilipokuwa nikijaribu kuuhifadhi. Ningewezaje kuishi katika jiji la Nairobi? Na isitoshe pesa walizonipa zilikuwa kidogo sana na mara nyingine walinipiga na kuniita mtoto. La. Sitakimbia tena. Msichana hawezi kuwa mbioni maisha yake yote.

Anaingia mvulana.

MVULANA: *[hajamwona msichana]:* Nimetahayari sana. Nilisahau maneno ya mwanamke: aliniambia nisimpige tena yule msichana. Hata sasa nahisi kama ambaye ananitazama, huku akiniapiza. Ninaona aibu sana.

SAUTI: Hata sasa u hayawani na msichana alisema kweli kukuita mnyama.

Msichana anachomoa kisu kutoka ndani ya skati yake, mvulana anamwona. Lakini ametubu hasa.

MVULANA: Sitaki kupigana nawe tena.

MSICHANA: *[sauti ya hasira]:* Mwoga!

MVULANA: Hakika kabisa.

MSICHANA: Mwoga.

MVULANA: Nataka kukuomba msamaha.

MSICHANA: Huo ni mtego. Mwoga, mchokozi, mnyama! Sitakukimbia tena. Sitakimbia asilani nionapo mtu yeyote.

Watazamana bila kusema lolote huku msichana akiwa anamwendea mvulana, kisu mkononi. Wanazungukana kama wanapimana nguvu.

MVULANA: Kiweke chini kisu hicho.

MSICHANA: Sasa jionyeshe kuwa u mwanamume kweli, mnyama we!

MVULANA: Nakwambia kiweke chini. Je unajua vile nitakavyokufanyia? Nitakushika nikuonyeshe kuwa sitaki tena kukuchezea. Sitaki tena pesa zangu. Unaweza kuwa nazo. Ulizihitaji kama nilivyozihitaji. Nilikuwa mjinga kupigana nawe kwa kutaka unilipe. Lakini usipoangusha kisu hicho . . .

MSICHANA: *[anajishika kiunoni na kumtemea mate mvulana]:* Waoga wote, wakorofi na wachokozi, wote wana tabia moja. Ukijifanya mwoga watakuonyesha cha mtema kuni. Unapokuwa shujaa na kujiweka tayari kwa kila jambo, wao huogopa na kujinyenyekea. Sasa bwana mkubwa, hebu jionyeshe kuwa kweli u mwanamume! Unamwogopa msichana?

Mvulana akiwa amedhurika kwa maneno haya anauweka chini mkate na kumwendea msichana bila uoga. Lakini naye yuko tayari na kisu chake. Wanazungukana wakitazamana miendo yao kwa uangalifu. Mara mvulana anamshika msichana ule mkono uliokamata kisu. Wanapambana. Mvulana anauzungusha mkono wa msichana wenye kisu na kumfanya akiangushe. Anakipiga teke na kukisukuma kwenye mkate. Wanaendelea kumenyana miereka. Mvulana anaweza kumwinua msichana lakini hawezi kumwangusha. Mara ghafla wote wawili wanaanguka chini. Wanajitahidi kufika palipo kisu na mkate. Mvulana anafikia kisu kwanza, anakitupa mbali. Msichana anamketia mvulana, halafu anashika mkate na kuutupa. Mkate unavunjika na bastola inatokeza. Wote wanaiona. Mara wanashikana kwa hofu. Wote wameghafilika. Mvulana anasimama na kuishika bastola kwa mikono ya kutetemeka huku akiichunguza.

MVULANA: *[kwa uchungu]:* Mwanamke. Mwuzaji matunda. Dedan Kimathi. Uongo mtupu. Sasa nimetambua yote.

MSICHANA: Umetambua nini?

MVULANA: Alitaka kuepukana na bastola hii na kunitia mashakani . . . Gerezani. Tena!

MSICHANA: Nini? Una maana gani?

MVULANA: Hebu sikiliza. Lazima unisaidie. Hatuna budi kusaidiana. Sasa nifanye nini na bastola hii?

MSICHANA: Lakini uliipataje?

MVULANA: Ni yule mwanamke. Nitatoa ripoti yote kwa Polisi. Sitaki kufa mie!

MSICHANA: Ukitoa ripoti, kwa kweli watakuua tu, watakuita gaidi!

MVULANA: Alaaniwe mwanamke yule.

SAUTI: Siku utakapoelewa kwa nini baba yako alikufa; siku utakapojiuliza kama ilikuwa ni haki kwake kufa kama alivyokufa; siku utakapojiuliza utafanya nini ili mtu mwingine asife kifo kama hicho; siku hiyo mwanangu, utakuwa umekuwa mwanamume.

[Mvulana anaonekana kama ametokewa na kitu cha ajabu.]

MSICHANA: Ni nini?

MVULANA: Hukumsikia?

MSICHANA: Nani?

MVULANA: Yule mwanamke.

MSICHANA: Lini? Wapi? Kwa nini unatetemeka jinsi hiyo?

[anamwuliza huku ameweka mkono wake begani pake.]

MVULANA: La, la, siyo sasa, mama.
Lakini nawezaje kukaidi mwito wake
Tena niendelee kuishi?

Shawishi la III

KIMATHI: *[kwa maumivu. Anagaragara]:* Nilijua aliyewafanya waje hawa wote. Mwenye benki . . . viwanda, . . . mlowezi, . . . gavana, . . . polisi, . . . jeshi, . . . hakimu, . . . wote ni wamoja. Walevi wa giza. Walevi wa damu. Ha! Ha! Kwa nini niwaogope? Wananchi watagundua tabasamu hizi . . . na urafiki huo ambao hawakuutazamia. Lakini je . . . ikiwa, itaniokoa maisha yangu? La . . . Ndoto . . . Vishawishi . . . Wananchi. *[anapiga kelele]:*
Watu wetu!

Anaingia Mkurugenzi wa Biashara-Mwaafrika bepari aliyevalia Kizungu, mwanasiasa na kasisi.

MKURUGENZI: Ndiyo, watu wetu, watu wako, watu wetu sote! Rangi nyeusi ni nzuri. Nguvu ya Mwafrika.

KIMATHI: Nafikiri nakufahamu. U nani wewe?
Nimekuwa nikikalia makaa ya mioto ya majaribu na vishawishi. Nitulizeni roho yangu ndugu zangu. Katika sehemu hii ndo-

go niliyofungwa ukutani, mtu anaweza kuwa mwenda wazimu.

MKURUGENZI: Unanifahamu sana. Nimekuwa nawe daima katika matatizo na mapambano. Wa Wachiuri, yamekuwa mapambano marefu. Nimetoa pesa kadha kwa juhudi za mapambano. Duka langu huko Masira lilikuwa kituo cha kulishia kiapo.

KIMATHI: Nafikiri nakujua, na wengine wa aina yako. Tumesafiri sote katika barabara hii ya mapambano. Ahsante. Wachache wetu, wamebaki nyuma. Walihadaiwa na adui na kuwa chini yake kama walinzi wake. Lakini kwa ujumla tumeshikana pamoja. Ahsante kwa msaada wako wa hundi kuyasaidia mapambano. Kutoka sasa tutakuwa tukiwafunza walimwengu kuhusu umoja.

MKURUGENZI: *[akohoa]:* Hiyo ndiyo sababu yangu kubwa ya kufika hapa. Sina wakati mwingi. Nataka kukuuliza: Je, wafikiri hatujashinda vita hii?

KIMATHI: Jinsi unavyonijaza matumaini kwa maneno yako! Kwa kweli tutashinda vita. Hebu niwaambie wale wasio na moyo wa kuendelea na mapambano kuwa juhudi zetu zitaendelea mpaka tutakaponyakua mamlaka ya kujifanyia mambo yetu wenyewe.

MKURUGENZI: Lakini, tayari tumekwisha faulu katika mapambano yetu.

KIMATHI: Katika moyo wa wananchi ndiyo. Katika moyo wao wa kutaka maisha ya uhuru na mamlaka . . . huo hauwezi kuangamia. Maneno yako ya imani katika mapambano ya wananchi yanaifanya minyororo hii iwe miepesi kama manyoya. Ningependa kuyasikia maneno hayo zaidi. . .

MKURUGENZI: *[bila kusubiri]:* Sikiza Dedan. Tumekwisha shinda katika vita hivi.

KIMATHI: *[ameshangazwa na maneno hayo]:* Wasemaje? Wadhalimu wetu wamejitolea? Tutawafukuza kutoka ardhi yetu, ardhi hii yetu ndugu zangu. Tuirekebishe hali yetu na kujenga taifa jipya. Maisha haya ya huzuni! Nanyi wabeba mikuki, mtakimbilia wapi mashujaa watakaporudi huku wakitangaza ushindi? Lakini wameshinda? Rafiki zangu, nawakaribisheni kwa mara nyingine kwa kuleta habari hizo nzuri. Moyo wangu umejaa kama mto Gura. Kweli wamekwisharudi? Mara moja hii? Ondoeni mi-

nyororo hii. Fungueni roho yangu! Fungueni karne nyingi za utumwa! Kenya yetu mpendwa, tuliyekununua kwa thamani kubwa!

MKURUGENZI: Si hivyo hasa, lakini hata hivyo kumekuwa na matangazo mawili muhimu, yamesema kuwa hakutakuwa tena na ubaguzi wa rangi hadharani, katika utawala, katika biashara, na katika mikopo. Na hata katika kunyakua ama kupata ardhi hakutakuwa na ubaguzi wowote. Wito mpya ni ushirikiano katika kuendeleza nchi hii. Je, si tumekuwa tukipigania mambo hayo? Kila Mwaafrika anayefanya kazi kwa bidii na anayo rasilimali anaweza kuwa bwana mkubwa. Tunaweza kuwa wakurugenzi wa makampuni ya kigeni. Tunaweza kununua ardhi katika nyanda za weupe. Nyanda za weupe zinaanza kumalizika. Swala kubwa ni mweupe akitaka kuuza ardhi yake Mwaafrika anaweza kuinunua akitoa bei itakikanayo.

KIMATHI: Ni usemi gani mpya huo?
Tununue ardhi yetu kutoka kwa wezi? Ardhi yetu? Kwani hatukuinunua kwa mito ya jasho la damu?

MKURUGENZI: Hakuna cha bure. Ubaguzi wa rangi umekwisha. Mabenki yako wazi kwa kila mtu. Tunataka nini zaidi ya haya?

KIMATHI: Na siasa? Uhuru? Je, mambo hayo pia yanauzwa?

MWANASIASA: Tumepewa mambo mawili ya kuchagua. Tunaweza kupata uhuru jimbo kwa jimbo. Majimbo. Kwa huruma yao kubwa wamekubali kuanzishwa kwa vyama vya siasa vya majimbo. Uhuru kwa Jimbo la Kati. Hata hivyo ni sisi Wakikuyu, Waembu na Wameru tuliopigania uhuru.

KIMATHI: Ungeweza kuviita vita vya ukombozi juhudi za jimbo moja? Ukoloni umeharibuje fikira zako? *[ananyamaza kidogo]*: Hebu nisikize. Kenya ni nchi moja ambayo haiwezi kugawanywa. Mapambano yetu si ya kukomboa jimbo moja bali kukomboa Kenya nzima. Haya ni mapambano ya wananchi.

MWANASIASA: Ala! Unaongea kama ambaye anaweza kusoma fikira zangu. Chaguo la pili tulilopewa ni kupewa uhuru kama taifa moja.

KIMATHI: Kupokea uhuru? Tangu lini watu wetu wamekuwa waombaji? Ni nani wewe? Unaweza kuwakatia kauli wananchi?

Wamewaachilia watu wetu kutoka kizuizini? Wamewaachilia Jomo Kenyatta? Paul Ngei? Fred Kubai? Wako wapi akina Achieng Oneko? Bildad Kaggia? Kungu Karumba? Wamekwisha achiliwa wote? Hebu nieleze!

MWANASIASA: Wataachiliwa hivi punde. Kwa sasa linalonihusu sana ni swala la kuachiliwa kwao. Kila mmoja anapigania kuachiliwa kwao. Tom Mboya, Ronald Ngala, Oginga Odinga, Daniel arap Moi, Julius Kiano. Kila mahali wanaongoza maandamano ya kupigania kuachiliwa kwa wale walio kizuizini. Baada ya hayo tutaunda chama cha siasa cha taifa zima na baadaye mashauri muhimu yataanza huko Uingereza. Tutaketi kujadili uhuru na bila shaka tutapewa uhuru wetu.

KIMATHI: Tupewe! Tupewe! Tupewe! Kwani sisi ni waombaji ambao tumenyoosha mikono yetu tayari kupewa? Hatuwezi kupewa uhuru katika sahani ya fedha. Ondokeni enyi viumbe waovu, panya wanyonyaji damu za watu wenu wenyewe! Damu ya wafanyakazi na wakulima wetu. Na sasa enyi wakulima wapya, makabaila wapya, wenye ngozi nyeusi lakini roho za kikabaila, mnataka kujinyakulia hekta elfu nyingi za ngano, michai, kahawa, pareto . . . mashamba ya kufugia ng'ombe . . . na huku wafanyakazi na wakulima wa vijishamba vidogo wanaishi kwa umasikini, bila ardhi!

Sasa nawafahamu watu ninyi!

Mnataka kuwa na hisa chache katika mabenki na makampuni, na kuiba kila muonacho ama mpatacho.

Mnataka kunyakua tu, na hali watu wengine hawana chochote. Ushirikiano katika maendeleo! Kwa mintaarafu gani? Utawafanyaje wajane, yatima na mamilioni wanaofanya kazi?

Mabwana wapya. Tuwachumie majani ya chai na kahawa yenu. Je, watu maskini wasio na hatia walikufa na wanaendelea kufa msituni kwa sababu hiyo?

Jemadari Kago, Baimunge, Matenjagwo . . . na mashujaa wengine bado wamefungwa . . . Stanley Mathenge. . . .

Umekuwa huko kuwasikia maoni yao, wanapojaribu kupigania Kenya mpya?

Mnasema tumeshinda, tumeshinda. Ni bei gani enyi wanywaji

wa asali kutoka kwa mafuvu ya vichwa vya watu?

MWANASIASA: Sote tulipigania uhuru kwa njia mbalimbali. Nafikiri si busara na ni siasa za kugawanya wananchi kwa kusema kuwa watu fulani walipigania uhuru. Hakuna ubaguzi Afrika. Sote tu wapigania uhuru.

KIMATHI: Ndiyo zawadi. Utumwa. Tutapata zawadi gani kwa kuwa watumwa kwa mara ya pili?

MKURUGENZI: Tukomeshe.

KIMATHI: Tukomeshe nini?

MWANASIASA: Vita msituni. Ahadi tulizopewa zatosha. Mpaka sasa wamekwisha kutupa viti kadha katika LEGCO. Huo peke yake ni ushindi mkubwa.

KIMATHI: Maneno. Maneno. Maneno. Huo ni mchezo wa kibalozi.

MKURUGENZI: Kiri hatia yako, uokoe maisha yako na maisha ya wengine. Ungana nasi.

KIMATHI: Akili zilizolaaniwa! Mapinduzi gani yatakomboa akili hizi? Tokeni. Tokeni watumwa wa akili.

[mkurugenzi na mwanasiasa wanatoka]:

Na wewe mtu wa ukosi mweupe? Wafuate wenzako mashambani. Wanyapara wapya wa mauaji ya wananchi.

PADRI: *[anatokea kwenye kivuli]:* Mwito wangu ni tofauti kidogo. Vitu vya dunia. Nyumbani kwa baba yangu mna makao mengi.

KIMATHI: Hata wewe baba yangu . . . Hebu niambie . . . unafikiri . . . la, lakini haiwezekani . . . ukifikiri, unaweza kufahamu kama watu wetu wangali wakipambana? Ama wameungana na adui kama wale wajinga wawili?

PADRI: Nimekueleza kuwa ufalme wangu si wa dunia hii.

KIMATHI: Usinikasirishe bure. Una maana gani kusema hivyo?

PADRI: Ulimwengu utakwisha na furaha zake zote, lakini neno la Mungu halitapita. Najua unaipenda Biblia . . .

[Padri anasoma vifungu kutoka kwenye Biblia kama ambaye ni Kimathi msituni. Anajifanya ameshikilia Biblia mikononi]:

Maombolezo, Sura ya 5, kifungu cha 1-9, "Ewe Bwana, kumbuka yaliyotupata, utazame na kuiona aibu yetu. Urithi wetu umegeuka kuwa mali ya wageni.

Na nyumba zetu kuwa mali ya makafiri.

Tumekuwa yatima tuliofiwa na baba;
Mama zetu wamekuwa kama wajane.
Tumekunywa maji yetu kwa fedha;
Kuni zetu twauziwa.
Watufuatiao wako juu ya shingo zetu;
Tumechoka tusipate raha yoyote.
Tumewapa Wamisri ardhi;
Na Waashuri pia, ili tushibe chakula.
Baba zetu walitenda dhambi, hata hawako;
Na sisi tumeyachukua maovu yao.
Watumwa wanatutawala:
Hakuna mtu wa kutuokoa na mikono yao.
Twapata chakula kwa kujihatarisha nafsi zetu;
Kwa sababu ya upanga wa nyikani."

KIMATHI: *[anaendelea kwa kukariri Mhubiri, Sura ya 4, Kifungu cha 1]:* "Kisha nikarudi, na kuona madhalimu yote yanayotendeka chini ya jua: na tazama machozi yao waliodhulumiwa na hawakuwa na mfariji. Na watesaji wao walikuwa na nguvu; lakini wao hawakuwa na mfariji." Kwa nini? Uliwezaje —

PADRI: Ni Biblia yako.

KIMATHI: Mimi husoma tu vifungu vile vinavyohusiana na mapambano yetu.

PADRI: Waona Dedan, hapo ndipo ulipokosea. Vifungu hivi haviongei juu ya mambo ya kilimwengu.
Ni mapambano ya kiroho. Mungu na sheria wanapopambana na roho zetu.

KIMATHI: Na wewe u nani?
Askari wa Injili? Mlinzi wa roho? Utaendelea hadi lini kuwa mtumwa wao?

PADRI: Umekosea tena! Sasa tunalifanya kanisa lisimamiwe na Waafrika wenyewe. Tunataka kumwona Kristo katika utamaduni wetu. Ngoma kanisani. Maaskofu Waafrika! Makadinali Waafrika na hata. . .

KIMATHI: Mtumwa mkubwa! Ni lini utakapotupilia mbali vazi hilo la kigeni na kuvaa vazi la Kiafrika kwa shughuli za kanisa? Padri, nieleze tofauti iliyoko baina ya mlowezi na Padri. Niambie!

PADRI: *[ameshangazwa]:* Kwa nini? Umewahi kuona mwanga, au si-vyo? Si ulibatizwa Dedan?

KIMATHI: Potelea mbali na jina hilo la Dedan. Mimi sasa ni Kimathi Wa Wachiuri . . . wa nasaba ya Iregi. Nimeona mwanga, lakini si aina ya mwanga uusemao. Nilikuwa nikitembea peke yangu. Nilikuwa nikitafakari katika vilele vya milima. Nimetembea na kutafakari katika ardhi iliyo kati ya Kirinyaga na Nyandarua.

PADRI: Ulikuwa daima mtu aliyekuwa pekee, usiyemwamini mtu yeyote. Mwishowe hata waganga wako mwenyewe walikuhaini. Kristo hawezi kumhaini mtu yeyote.

KIMATHI: Uhaini. Uhaini. Manabii.

Nimekuwa siwaamini wale wanaohutubu amani na huku kuna udhalimu. Geuza shavu jingine!

Usiwapinge wale wanaovaa kama vipepeo! Wasaliti!

PADRI: Toa roho yako kwa Kristo, Dedan, mruhusu Yesu aongee nawe leo.

KIMATHI: *[akiendelea na hotuba yake]:* Nimezungumza na Mungu wa babu zangu katika ndoto na juu ya milima, na hata mara moja Mungu huyo hakunitaka nitoe roho yangu.

Siku moja, nilipokuwa nikitazama milima, huku nikisikiza maporomoko ya mto Gura, nilifikiria juhudi za watu wetu, wale ambao wamekuwa wakipinga udhalimu, nilifikiri niliona sura mpya ya Kenya itakayokuja: Wafanya kazi wakiungana mikono kutoka Pwani hadi Ziwa Viktoria, na kufanya mito, milima na radi mawinguni, kuwafanya mabwana na maumbile waweze kuwatii. Mtu ni mtumwa wa maumbile? La, maumbile ni mtumwa wa mtu, na kumfanya mtu asiwe mtumwa wa mtu mwingine. Sauti zilinijia na nikasikia sauti kuu ya Wakenya:

Uacheni upepo uvume,
Acheni mvua inyeshe,
Mito, mikono ya mito, maporomoko yatumieni,
Yatumieni kwa manufaa yenu.
Majangwa yastawisheni.
Tumieni nguvu za maumbile ipasavyo, na hapo mtakuwa watoto wa Mungu-wajenzi wa mbingu mpya katika ardhi mpya.

PADRI: Usikufuru. Ulisema uliwaogopa na kupigana na wakuu wa kanisa?

KIMATHI: Nilihofu kuwa wale wanaojitangaza kuwa mitume wa Mungu wangekuja kwa wazalendo na kusema: jitoeni . . . ndivyo Mungu asemavyo.

PADRI: Na wafikiri wakati wa kufanya hivyo haujawadia?

KIMATHI: Ala! Hata wewe pia?

PADRI: Jitoe! Komesha umwagikaji wa damu. Maisha mapya, maisha ya uhusiano mpya katika Kristo.

KIMATHI: Na damu tuliyomwaga je? Ilikuwa kazi ya bure?

PADRI: Sote tumefanya dhambi na kumkosea Mungu. Kwa nini upoteze maisha ya watu zaidi? Kiri makosa yako na umwombe Mungu msamaha.

KIMATHI: Kwani ni dhambi hata mbele ya Mungu wako kwa watu kupambana na wanyonyaji? Mtoe ibilisi kichwani mwako na uniambie dhahiri ewe mzee, kama watu walioapa kupigana na udhalimu wanaweza wakakata shauri kuvunja kiapo chao?

PADRI: Fikiria maneno yangu mwanangu. Kuna busara ndani yake. Niliyokwambia yatosha.

KIMATHI: Haya ndiyo niliyokuwa nikihofia,
Namna ya kuwavisha adui zetu,
Nguo nyeusi na kuwapa ndimi tamu,
Wanamapinduzi wanaotumia hundi!
Nenda. Nenda. Majaribu yangu yameanza.
[Padri anaendelea kuketi]: Nilikwambia utoke! La, usitoke *[ananyamaza kidogo]:* Toka. Njoo katika mahakama ya bandia kesho. Utasikia jibu langu. Kesho . . . kesho . . . nilikwambia uende.

Padri anatoka.

Ni nani rafiki na ni yupi adui?
Jamani, uchungu wa vita vya mtu binafsi!
Lakini nitapigana hadi mwisho
Pekee. . . .
Nilisema pekee? La, Toa mashaka hayo.

Barabara

Siku ile ile, magharibi — karibu jioni. Mvulana na msichana

wanaweza kuona lango la gereza. Mlinzi yupo langoni. Mvulana na msichana wanaota gereza.

MVULANA: Hebu tazama: kuna mlinzi wa gereza, anatembea juu na chini.

MSICHANA: Bila shaka lazima kuweko na mlinzi. Ulitegemea kuikuta milango yote wazi bila walinzi ili kila mtu aweze kuingia ndani? Twende tukaongee naye yule mlinzi.

MLINZI: Ondokeni. Mwafikiri mnakwenda wapi?

MVULANA: Tafadhali bwana mkubwa, umemwona mtu anayeuza machungwa hapa?

MLINZI: Hapa? Jioni hii? Ni nani angeyanunua? Nendeni zenu.

[Mvulana na msichana wanarudi nyuma hatua chache.]

MVULANA: Nimechoka kuibeba. Ni heri tuitupe ndani ya choo ama msituni na tusahau.

MSICHANA: Wafikiri hivyo ndivyo kuwa mtu mzima? Si saa chache tu uliniambia mwanamke alivyokuambia? Wakati huo ulikuwa na moyo na matumaini. Umekwisha sahau ahadi tuliyoweka saa moja tu iliyopita?

MLINZI: Ninyi hapo! Nimewaambia mwende zenu.

MVULANA: Huyu ni katili. Lakini tumemkosaje mwuza matunda?

MSICHANA: Tusimfikirie mwuzaji ama mwanamke bali tujifikirie sisi wenyewe vile tutakavyofanya.

MVULANA: Namna gani?

MSICHANA: Kwanza tuna bastola.

MVULANA: Umeiweka vizuri rindani mwako?

MSICHANA: Usiwe na shaka. Kwa kweli hatuwezi kumwona mwuzaji matunda.

MVULANA: Hivyo ni wazi kabisa.

MSICHANA: Hatuwezi kumwona mwanamke vile vile.

MVULANA: Kwani hayo sijui?

MSICHANA: Lakini ngoja nikuulize. Kwa nini mwanamke akakutaka umpe mkate mwuzaji matunda?

MVULANA: Siwezi kujua kwani sikumwuliza.

MSICHANA: Ni dhahiri kwamba kulikuwa na mpango wa kumwokoa Kimathi. Alikuambia jinsi Kimathi alivyokuwa karibu kuokole-

wa huko Ihururu. Bastola hiyo aliyokupa ilipangwa apewe Kimathi.

MVULANA: Ndiyo . . . ndiyo.

MSICHANA: Jambo ni kwamba, mpango huo uliharibika. Na sasa wataka tufanye nini?

MVULANA: Hata mimi najiuliza swali hilo hilo.

MSICHANA: Tutekeleze mpango huo sisi wenyewe. Ni lazima tumwokoe Kimathi.

MVULANA: Una wazimu nini?

MSICHANA: Lakini ni lazima tumwokoe. Umeongea juu ya mwito. Huo ndio mwito alioutaja yule mwanamke.

MVULANA: Ndiyo. Mwito. Na aliongea juu yake kama ambaye alikuwa akinijaribu. Alisema siku moja utagundua kwamba kumpiga mwenzio hakutakufanya kuwa mtu mzima. Ndiyo kabisa. Tumwokoe Kimathi. Lakini vipi?

MSICHANA: Tununue mkate na tuitie bastola ndani yake. Tumletee mlinzi ambaye atampa Kimathi, na hapo Kimathi ataweza kujiokoa kwa urahisi.

MLINZI: Bado hamjaondoka? Acheni kupiga kelele na kuchezacheza bure.

MVULANA: Huyu ni mkorofi nakwambia. Tukimbie ili tupange tutakavyotekeleza mpango wetu halafu turudi . . . lakini atatukumbuka.

MSICHANA: Najua tutakavyofanya. Tutavalia nguo za kuficha asili yetu.

MLINZI: *[akiwakaribia]:* Nitakupigeni risasi ama kuwafungia ndani gerezani. *[wanakimbia]:* Huyu mfungwa . . . damu mbaya kabisa. Tangu niingie zamu sijapumzika hata kidogo. Watu . . . wanakuja na kuondoka . . . na mfungwa amefungiwa na kulindwa imara. Kama ningekuwa wao, nisingejishughulisha na kesi. Ningemvunja shingo. Anaingia mwanamke aliyevalia kama muuza matunda.

MLINZI: Wewe! Wewe muuza matunda!

MWANAMKE: Machungwa ni rahisi leo, wataka kununua moja?

MLINZI: Kuna mvulana na msichana wanaokutafuta.

MWANAMKE: Mvulana na msichana? Walikuwa wamebeba kitu chochote?

MLINZI: La, hawakubeba kitu. Kwa nini wauliza hivyo?

MWANAMKE: Walifuata njia gani?

MLINZI: Njia waliyojia.

MWANAMKE: Si neno. Hebu niambie bwana mlinzi. Yuko wapi yule mlinzi aliyekuwako kabla ya wewe? Nilikuja mapema leo lakini sikumkuta.

MLINZI: Nitajuaje? Kila kitu kimegeuka. Sote hapa tu wageni. Tangu jana. Wanaendelea kubadilibadili walinzi. Naona sababu kubwa ni juu ya usalama wa huyu mfungwa . . . Kimathi. Damu mbaya kabisa. Wana hofu kuwa huenda kukafanywa mpango wa kumwokoa kwa kutumia silaha. Jana usiku wafuasi wa Kimathi waliokuwa na silaha za kujitengenezea wenyewe walishambulia Ihururu. Damu mbaya kabisa . . . kama ningekuwa wao ninge— *[anachukua machungwa kutoka kikapuni mwa mwanamke na anatoa sarafu moja na kumrushia.]*

MWANAMKE: Usinilipe. Labda nitakaporudi?

[anatoka.]

Shawishi la IV

Kuna giza katika chumba cha gereza alimo Kimathi. Anaonekana ameketi katika pembe yake aliyoizoea akijaribu kupata mwangaza kutoka dirisha dogo lililo juu ambalo limezungushiwa seng'enge. Anapiga mbinja kuigiza wimbo mmoja wa mapambano huku akiwa katika hali ya kufikiri. Mara anasikia mlio wa viatu ukiandamana na filimbi. Walinzi wanapiga saluti na Shaw Henderson anapita kati yao ameandamana na Waitina na askari wawili wa KAR wenye silaha, askari wa kwanza na wa pili. Wanapoingia Kimathi hageuki kuwatazama.

HENDERSON: Fungua, upesi! Nataka kutoa heshima zangu za mwisho kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dedan Kimathi.

Walinzi na Askari wa Pili wanaangua kicheko. Askari wa Kwanza anaonyesha huzuni. Mlango unafunguliwa na Henderson anaingia kwa dharau.

HENDERSON: *[kwa mzaha]:* Wajionaje na hali leo Jemadari?

KIMATHI: Kama kawaida *[bado hajamtazama]:* Wajumbe wako wameniondolea ukungu machoni mwangu. Sasa naweza kuongea kwa uthabiti zaidi na uhakika. Naona—

HENDERSON: Amka Kimathi. Achilia mbali njozi.

KIMATHI: *[anageuka kumtazama Henderson kwa chuki]:* Unataka nini zaidi kutoka kwangu? Niuze watu wangu . . . ardhi . . . roho yangu. Kwa nishani kutoka kwa Mfalme George, ama Malkia? *[kwa mkazo]:* Shaw Henderson! Mchuuzi wa maisha ya watu!

[Waitina yuko tayari kumzaba kibao lakini anazuiliwa na Henderson. Kimathi anaendelea bila wasiwasi]: Ndiyo. Unajifanya mkombozi wa watu wetu. Hebu sikiliza kwa makini. Nitapigana hadi nione mwisho wake. Kuilinda ardhi yetu na kuwalinda watu wetu.Hivyo ndivyo nilivyoapa mimi Kimathi waWachiuri.

HENDERSON: Itabidi ufanye hivyo toka kwenye kitanzi Jemadari.

KIMATHI: Nimekwishahukumiwa sivyo? Hivyo ndivyo haki ya sheria ya Kiingereza ilivyo! *[anacheka kwa sauti na kwa dharau.]*

HENDERSON: *[akiwa ametahayari]:* Sikiza wewe mwenda wazimu. Sitaweza kuvumilia upuzi kutoka kwa haramia kama wewe. *[Kimathi anamtazama bila kupepesa macho]:* Nimefanya kila nililoweza kukuponya maisha yako. Serikali hii ya kidemokrasia haiwezi kuendelea kuvumilia upumbavu wako. Wewe mwenyewe huonekani kama unapenda kusaidiwa. Basi vile unavyolichukua swala hili, ndivyo utakavyotendewa.

KIMATHI: Hifadhi vitisho vyako kwa mwoga mwingine, siyo mimi. Unapoteza pumzi zako bure.

HENDERSON: *[kwa hasira]:* Nyamaza ama nitakupiga risasi mumu humu gerezani. Nitakupa nafasi ya mwisho Kimathi. Yuko wapi Mathenge?

KIMATHI: *[kwa dharau]:* Wataka niseme nini kwa swali lako? Aah, yuko huko msituni. Katika msitu wa Nyandarua ama Kirinyaga. Anapambana na majeshi yenu. Ama unataka niingie katika moja ya ndege zenu huku nikipayuka: Jisalimisheni! Jisalimisheni! Jisalimisheni!

HENDERSON: *[akiwa amepandwa na hasira]:* Nakupa nafasi nyingine

na ujihadhari jinsi utakavyonijibu. Stanley Mathenge yuko wapi?

KIMATHI: Nafasi ya pili ya mwisho? *[kwa dharau]:* Ndiyo. Haki ya sheria za Kiingereza. Sikiza, hakuna sababu Shaw Hender . . .

HENDERSON: *[anampiga kofi Kimathi]:* Askari!

ASKARI: *[akipiga saluti]:* Afande!

Kimathi anacheka kicheko cha dharau. Anamtazama Askari wa Pili kwa jicho baya halafu anatema mate chini kwa hasira.

KIMATHI: Panya!

HENDERSON: *[anamchapa kibao tena]:* Hapa siyo msituni kwenye Himaya yako. Lizingatie hilo.

KIMATHI: *[anamtazama kwa chuki]:* Kama unajua kupigana nifungue sasa. Tuonane uso kwa uso kama wanaume. Tuone ni yupi hodari kwa miereka, mwoga wewe.

Sasa Henderson akiwa na hasira kama mnyama aliyejeruhiwa, anamchapa Kimathi kila mahali akitumia bunduki, ngumi na mateke.

KIMATHI: Endelea kunichapa tu Shaw Henderson, mwuzaji wa binadamu! *[mara Kimathi hawezi kustahimili tena mapigo ya Henderson na anajaribu kuikata minyororo yake]:* Mwoga, mkorofi wee! Kuna mtu aina yako aliyepigana vita na mtu wa rika lake?

HENDERSON: *[anatoka huku akipiga makelele]:* Askari, mtoe umpeleke chumba cha mateso. Mwambie Gatotia afanye kazi yake barabara. Haraka!

ASKARI WA PILI: Ndiyo, afande! *[anamsukuma Kimathi kuelekea chumba cha mateso.]*

ASKARI WA KWANZA: *[akihuzunishwa na kitendo hicho]:* Wewe u mwanadamu ama mnyama? Kwa nini ufanye hivyo?

Askari wa pili anageuka kama kwamba anataka kujibu lakini anaendelea na kazi yake.

HENDERSON: *[akionekana katika mlango wa pili wa chumba cha mateso]:* Mwanaharamu. Mwafrika mpumbavu. Hiki kiapo kimewaharibu vichwa. *[kwa sauti ya kuamuru]:* Mko tayari? Haya basi, Gatotia, anza kazi yako. Bwana Waitina atakueleza

ni wakati gani na ni mahali gani ufanye nini.

WAITINA: *[kwa hamu kubwa]:* Usijisumbue bure. Nitaendesha mwenyewe mateso. *[anamkaribia Kimathi]:* Lala chini hapa.

Waitina anakunja mikono ya shati lake na kukamata mjeledi kwa furaha kubwa. Gatotia na askari wa pili wanamvua shati Kimathi na kumlaza chini akiwa na minyororo yake. Waitina anaponyosha mkono kuanza mateso, mara taa zazima na watu wanasikia tu mlio wa mjeledi. Katika nusu mwangaza, tunaona marudio ya maonyesho ya historia ya Mwafrika yaliyofanywa hapo mapema.

WAITINA: *[anamchapa na huku anamuuliza maswali]:* Yuko wapi Mathenge? Katika misitu yako amejificha wapi Stanley Mathenge? Matenjagwo? Wapi? Sema.

[Kimathi anasikia uchungu mkubwa]: Vizuri, anataka kusema sasa. Gatotia, acha sasa. Mwache aongee.

KIMATHI: *[anaongea na Gatotia]:* Utapata nishani gani kwa kazi hii yako wewe msaliti mkubwa?

WAITINA: Endelea, Gatotia! Mfunze adabu. *[anamchapa viboko zaidi]:* Acha sasa Gatotia. Je, Jemadari uko tayari kuongea? *[Kimathi anaendelea kusikia uchungu mkubwa]:* Gatotia!

GATOTIA: Afande!

WAITINA: Sasa mtese kwa nguvu za umeme.

GATOTIA: Ndiyo afande.

WAITINA: *[amchapa kibao usoni]:* Wako wapi Mathenge, Matenjagwo na maharamia waliobakia? *[anampiga kofi]*: Tia sahihi karatasi hii na waambie wajisalimishe kwa jeshi la Kiingereza.

KIMATHI: Sitafanya jambo kama *hilo* asilani.

WAITINA: Vizuri. Nitakuonyesha . . .

Kunasikika kilio cha huzuni katika chumba cha mateso; Kimathi aliyetapakaa damu mwili mzima anasukumwa kutoka chumba cha mateso na kuanguka, angali amefungwa minyororo. Henderson, Waitina na Gatotia wanatokeza wakiwa wamebeba vyombo vya kutesea. Wanasimama pamoja isipokuwa yule askari mwenye huruma ambaye anajitenga nao. Ingawa Kimathi ameumizwa, dhamira yake iko imara.

HENDERSON: Sasa tia sahihi *[Kimya.]* Tia sahihi — jitolee.

Anamrushia Kimathi kipande cha karatasi. Kinaanguka sakafuni. Kimathi anajaribu kuinuka na kuwahutubia Gatotia na askari wa Kiafrika.

KIMATHI: *[akiongea kwa uchungu]:* Nyinyi . . . wasaliti wa watu wenu wenyewe . . . Wauzaji wa watu wenu wenyewe . . . Mtapata nini
Kwa ulafi wenu wenyewe.
Mpate kuketi meza moja na bwana mkubwa.
Mpate akiba ya benki. Mshirikiane katika biashara. Ushirikiano?
Wa kuwanyonya watu wenu wenyewe . . . kuwanyonga watu wenu wenyewe . . . mpate nishani na makombo! Watu wetu hawatawasahau kamwe wasaliti nyinyi mliojinenepesha. *[anachukua kipande cha karatasi]*: Kipande hiki Henderson . . . *[anasita]:* Kwa miaka mia nne mdhalimu amekuwa akiwanyanyasa watu wetu na kuwatesa.
Kwa miaka mia nne tumepambana na udhalimu, kunyanyaswa, utumwa, kutekwa akili, roho na miili yetu.
[akikipasua kipande kile cha karatasi]: Watu wetu hawatajisalimisha kamwe! *[anavitupa vipande vya karatasi usoni mwa Henderson.]*

HENDERSON: Gatotia! Askari! Mrudisheni katika chumba cha mateso.

ONYESHO LA TATU

Barabarani mjini Nyeri, siku ya pili

Mapambazuko. Kuna mwangaza wa kiasi na ndege wanasikika wakiimba mitini. Wanaingia mvulana na msichana, wamevalia Kimasai. Wanaelekea kwenye lango la gereza.

MLINZI: Simameni! Mwataka nini?
MVULANA: Tunataka kumwona mfungwa.

MLINZI: *[kwa ukali]:* Mfungwa yupi? Ondokeni. Hapa si manyatta ya Kimasai.

MVULANA: Lakini mfungwa yumo humo ndani . . . Kimathi.

MLINZI: Maajabu kweli hayataisha. Wamasai? Kimathi? Mnataka kumdanganya nani? Nendeni zenu.

MSICHANA: Tunataka kumsalimia tu na kumpa mkate huu.

MLINZI: Mkate kwa Kimathi? Uliteni hapa. Mna uhusiano gani na Kimathi? Wapiganiaji wa uhuru? Haya, si neno. Nimekuwa hapa bila chakula usiku kucha. Asanteni kwa mkate.

MVULANA NA MSICHANA: Hatukukuletea wewe!

Mara kwa ghafla kunasikika ngurumo za pikipiki, ving'ora vya polisi na ngurumo za ndege.

SAUTI: Liprightlipright . . . attention!

Kunasikika hatua zinazoelekea kwenye lango la gereza. Mlinzi anautupa chini mkate na kuokotwa na msichana na mvulana. Halafu wanasimama kando na kutazama juu angani. Wanasikia ngurumo za ndege. Kunasikika kelele za mtu karibu na pale walipo. Wanakimbia nje. Anaingia mwanamke ambaye angali anavalia kama mwuzaji matunda. Mara msichana na mvulana wanatokeza kutoka upande wa pili. Wanagongana.

MVULANA NA MSICHANA: *[kwa mshangao]:* Mwuzaji matunda!

MWANAMKE: Machungwa rahisi leo — Jamani ni ajabu kuwaona Wamasai Nyeri!

MSICHANA: *[anamkaribia]:* Samahani, Bwana Mwuzaji Matunda.

MWANAMKE: Naam.

MSICHANA: Tulitumwa tukuletee mkate. *[mara mwanamke anawakumbuka na kucheka.]*

MWANAMKE: Maajabu hayatakoma. Karibu nishindwe kuwatambua.

MSICHANA NA MVULANA: Ni yule mwanamke!

MWANAMKE: Sssssch! Nifuateni mahali faraghani tuzungumze.

Wanaondoka na kwenda mahali pembeni. Mvulana na msichana wanaketi miguuni pa mwanamke. Mwanamke ajifanye mwakilishi wa wanawake wote wanaofanya kazi wanapoongea na watoto wao.

MWANAMKE: Tutaketi hapa ambapo tunaweza kuwaona wakimchukua. Je, mngali mnao ule mkate?

MVULANA: Kwa mini ulinifanyia ujanja wa kubeba bastola?

MWANAMKE: Kumbe uligundua? Nilifikiri ulisema uko tayari kula kiapo. Mwanangu, nilikuambia kuwa wewe sasa ni mtu mzima na wala si mtoto tena. Sikutarajii kuwa kijana milele, wala hatuwatarajii vijana wetu kuwa waoga. Uliona hofu?

MSICHANA: Aliogopa sana!

MVULANA: Niliogopa kweli . . . lakini huyu msichana . . . hakuwa hata na chembe ya woga.

MWANAMKE: *[akiona fahari]:* Hivyo ndivyo inavyofaa kuwa. Badala ya kupigana ni lazima tushirikiane kuangamiza unyonyaji na udhalimu. Ni lazima tufarijiane mpaka tuupate ushindi.

MSICHANA: *[akiwa na shaka]:* Ni vigumu sana kutokana na udhaifu wetu.

MWANAMKE: Tukiwa na umoja, nguvu yetu inakuwa imani ambayo yaweza kuhamisha milima.

MVULANA: Kwa nini ulijitokeza ghafla ukiwa umevalia kiume?

MWANAMKE: Katika mapambano ni lazima uwe tayari kujibadilishabadilisha kulingana na hali ilivyo. Jana ilikuwa siku ya mikasa kwetu. Kwanza kuhojiwa na kufanyiwa uchunguzi, halafu hao Johnnie! Nilishtukia mtutu wa bunduki! Halafu baada ya kuachana nanyi niligundua kuwa mwuzaji matunda alikuwa mmoja wa wale waliotiwa mbaroni jana katika uvamizi uliofanywa na adui.

Huyo alikuwa mtu muhimu sana katika shughuli zetu za mapambano. Jambo hilo limeharibu mipango yetu kabisa. Ningefanya nini? Nilivalia kama mwuzaji matunda ili iwe rahisi kwenu kunitambua. Kesi iliahirishwa mapema kuliko nilivyotazamia: Basi ikanibidi kufuata halaiki ya watu. Nilitazamia kuzungumza na mlinzi wa gereza, ambaye pia ni mtu aliye upande wetu. Niligundua kuwa naye alikuwa hayupo, amehamishwa. Sasa ikawa mawazo yangu na imani yetu yote iko kwako. Niliendelea kukutafuta kila mahali, kati ya hapa na majengo hapana mahali sijapakanyaga. Ni hatari kubwa: lakini jambo likianzishwa lazima likamilishwe.

MSICHANA: Sasa utafanya nini wewe peke yako?

MWANAMKE: *[akiwatazama msichana na mvulana]:* Siko peke yangu. Niko nanyi!

MSICHANA: *[akiruka kwa furaha]:* Niko tayari!

MVUALANA: *[naye akiruka]:* Hata mimi pia niko tayari! Lakini wataka tufanye nini?

MWANAMKE: *[akifikiri]* Hebu sikizeni. Kimathi ni bingwa katika mapambano haya yetu. Kwa hivyo ni muhimu aokolewe hata kama tutapoteza watu kadha. Mapambano lazima yaendelee. Sasa hivi watamchukua wampeleke mahakamani. Nitaingia ndani nimevalia mavazi ya kutisha. Halafu nanyi mnifuate. Nitaongea na Kimathi kwa macho.

Nitakapokohoa, mtaanza kufyatua risasi. Katika ghasia hizo Kimathi atanifuata. Tokeo kama hilo la ghafla laweza kufanya miujiza. Wakati fulani mashujaa watano walipambana mpaka kituo kimoja cha Walinzi wa Majumbani kikajisalimisha. Mambo yote yanategemea vile yatakavyopangwa: Baada ya hapo itakuwa kazi rahisi. Tunaweza kuelekea Majengo. Tukifika huko hakuna mtu atakayeweza tena kutupata.

MVUALANA: *[akiwa na furaha]:* Trrrrrrrrr! Trrrrrrrrr!

MSICHANA: Trrrrrrrrrr *[wanaigiza watakavyomwokoa Kimathi]:* Lakini Dedan Kimathi ni nani hasa?

MWANAMKE: Kiongozi wa wasio na ardhi. Kiongozi wa wale wanaochubuka kwa kazi.

MVULANA: Tunajuaje kuwa aliyeshikwa ni Kimathi hasa na wala si mtu mwingine?

MSICHANA: Mimi siamini kabisa! Kwa sababu Kimathi angekuwa ametoroka mara moja. Nimesikia habari ya vile alivyomwandikia barua gavana siku moja. Alisema angekula naye katika Ikulu yake. Gavana aliwachukua askari wote toka Nairobi waje kumkamata Kimathi. Lakini Kimathi alikwenda hapo akiwa amevalia kama Inspekta wa Polisi wa Kizungu. Baadaye alimwandikia barua tena Gavana iliyosema, "Ahsante sana kwa chakula cha jana usiku." Na barua hiyo ilikuwa na sahihi ya: Jemadari D.K.

MVULANA: Hata mimi nimewahi kusikia kuwa aliweza kujigeuza ndege. Na pia kabla ya kushambulia kikosi cha adui, angeenda

katika kambi ya kikosi hicho na kupiga tarumbeta.

MSICHANA: Na kwamba aliweza kutambaa kwa tumbo kwa maili mia moja —

MVUALANA: Kwamba aliweza kucheka kwakwa na wala adui walio karibu hawakuweza kusikia kwakwa zake.

MSICHANA: Kwamba aliweza kuigiza milio ama sauti ya mnyama yoyote na watu wasiweze kutofautisha.

MVUALANA: Sasa wangewezaje kumkamata?

MSICHANA: Wamekamata kivuli chake.

MWANAMKE: *[kwa makini]:* Ni kweli wanangu kuwa Kimathi aliweza kufanya maajabu. Hata sasa wananchi wangali wakisimulia juu ya mapigano yake huko Mathari, Mlima Kenya na Naivasha. Ndiyo. Watu wanasimulia vile alivyoweza kuziangusha ndege za adui kwa mtondoo! Alikuwa mwalimu halisi, mwenye kuwachekesha watu wote. Aliweza pia kuigiza mtu yeyote ulimwenguni. Alikuwa msimulizi mkubwa wa hadithi zilizowatuliza mashujaa wenzake msituni. Lakini mbali na haya yote, aliwapenda wananchi na nchi yake. Alichukizwa sana na kitendo cha Waafrika kuwaua wenzao hata akalegeza msimamo wake kwa adui yetu. *[pole pole]:* Ingawa alikuwa kiongozi mkubwa ambaye daima hakuwa mwoga, pia alikuwa mwanadamu mwenye huruma! [*kwa hasira*]: Binadamu hasa.

Msitu wa Nyandarua: Kambi ya Mashujaa

Mwanamke amalizapo maneno yake, jukwaa linabadilika na kuwa mahakama pamoja na mkutano mkuu msituni. Sasa tunawaona wapigania uhuru wakiingia jukwaani wakiimba wimbo wa Kimathi.

"Rwimbo Rwa Kimathi":

Kimathi wetu alipopanda
Mlimani pekee
Aliomba nguvu na ushujaa
Kumshindia Mzungu

Alitutaka tufuate
Mapito yake aliyopitia
Njia zake alizoshika
Na tuwe na ushujaa kama wake.

Ukifuata njia hii
Niliyofuata mimi mwenyewe
Utakutana na matatizo
Lakini mwisho wake ni uhuru. . . .

Anaingia Kimathi akifuatwa na majemadari wengine: Njama, Matenjagwo, Mbaria Kahiu, Kimemia, Ole Kisio, n.k. na mwanamke.

KIMATHI: Njama!
NJAMA: Jemadari!
KIMATHI: Shika kalamu yako *[akimgeukia Matenjagwo]:* Matenjagwo, Ole Kisio!
MATENJAGWO NA OLE KISIO: Jemadari!
KIMATHI: Mmeweka walinzi kila upande?
OLE KISIO: Ndiyo, Jemadari.
MATENJAGWO: Katika eneo la maili mbili za mraba. Kila sehemu muhimu.
KIMATHI: Kimbo! Mbaria!
KIMBO NA MBARIA: Jemadari!
KIMATHI: Waleteni wauaji! Waleteni askari wa kukodiwa.

Askari wawili Wazungu na askari Mwafrika wa KAR wanaletwa mbele, mikono yao imefungwa nyuma.

KIMATHI: *[kwa askari wa Kizungu]:* Kikosi chenu?
ASKARI WA KWANZA NA WA PILI WA KIZUNGU: Lincoln Fusillers
KIMATHI: Majina yenu?
ASKARI WA KWANZA: Winterbottom!
ASKARI WA PILI: Smith!
KIMATHI: Kutoka wapi?
ASKARI WA KWANZA: Scotland . . . Dundee.
ASKARI WA PILI: Southampton, Uingereza.
KIMATHI: Wazazi wenu ni matajiri ama ni wafanyakazi?

ASKARI WA KWANZA: Masikini. Sisi ni masikini. Wafanya kazi tu.
KIMATHI: Mnawapigania wafanya kazi wa nchi yenu?
ASKARI: *[Wanatazamana kwa mshangao kama wasioelewa analosema.]*
KIMATHI: Mambo ni yale yale. Watu masikini wanapelekwa vitani wafe ili kuwanufaisha wanyonyaji. Fahamuni kuwa hatupigani vita hivi na Waingereza. Tunapinga ukoloni na ukabaila wa Waingereza waliotunyang'anya ardhi yetu, viwanda vyetu na utajiri wetu. Je, mko tayari kuhaini ukabaila wa Waingereza?
ASKARI: *[wakisimama imara]:* Sisi ni askari wa Malkia!
KIMATHI: *[kwa hasira]:* Upuzi huu wa kikabaila unaifanya damu yangu iyeyuke kwa hasira. Mliifanya safari hii yote, maili nyingi kutoka kwenu, kuwaua watu wetu, ili *Lord* fulani aendelee kuwanyonya baba zenu kwa amani?
ASKARI WA KWANZA: Tulikuwa tunaitii amri tu —
KIMATHI: Amri ya kuwaua –
UMATI: Wauawe . . . Wanyonge wawakilishi wa wakoloni!
KIMATHI: *[kwa hasira]:* Tokeni, nyoka nyie! Wachukueni.
[anamgeukia askari Mwafrika]: Na wewe je? Waonekana kama mmoja wetu.
ASKARI WA KAR: Kweli, ni mtu mweusi kama nyinyi. Usiniue ndugu!
KIMATHI: Na unapigana nasi? Askari wa kukodiwa! Ulipigana vita Burma kudumisha ukoloni! Ukapigana vita vya Japan kwa niaba yao!
Na sasa unapigana vita kwa niaba yao, kuwaua watu wako? Kinyume cha matakwa ya watu wako! Wanakulipaje?
ASKARI WA KAR: Shilingi mia moja.
KIMATHI: Kwa mwezi? Ni hilo tu?
ASKARI WA KAR: Pamoja na posho!
KIMATHI: *[akicheka]:* Ni hivyo tu?
ASKARI WA KAR: Basi.
KIMATHI: Na kwa kiasi hicho tu unawaua watu wako? Nilidhani wangekuhonga zaidi! Hisa katika makampuni ya magari.
Hisa katika biashara mbalimbali.
Hisa katika Hoteli za watalii,
Hisa katika mashamba yao ya ngano

Hisa katika utajiri wao wa wizi.
Hizo tu?
Na kwa shilingi mia moja
Na posho
Na nishani
Unawasaidia kuuwa na kuiba mali zetu! Uko tayari hata kufa ukiwatumikia?

Milio ya risasi inasikika.

ASKARI WA KAR: *[akiwa na hofu]:* Nisamehe, nionee huruma ndugu yangu.

KIMATHI: *[kwa huzuni]:* Mchukueni. *[kwa ghadhabu]:* Mwondoeni huyu askari wa kukodiwa.

Askari anaondolewa.

KIMATHI: Chonjo!

Kunasikika milio mingine ya risasi halafu kilio.

KIMATHI: Chonjo. Tuwe chonjo kila wakati.
Karibuni tena, mashujaaa ndugu zangu, katika mkutano wetu wa mwisho.
Kwa siku tatu sasa, tumejadili mambo mengi
Yanayohusiana na mapambano yetu. Tangu tuunde majeshi yetu sita:
Jeshi la Ituma Ndemi,
Jeshi la Gikuyu Iregi,
Jeshi la Kenya Inoro,
Jeshi la Mei Mathani,
Vikosi vya Townwatch,
Jeshi la Levellation,
Tumenyakua ushindi mkubwa. Maadui wetu popote Kenya. Hawapati lepe la usingizi. Hivyo sasa wamewaleta Majemadari wao hodari:
Lathbury, Hinde, Erskine
Na pia
Ndege zao za kisasa za kivita

Inaonyesha dhahiri kuwa tumewaumiza pabaya.
Sasa yatupasa tumshambulie adui kutosha pande zote
Tumepeleka wajumbe kuwashawishi mashujaa kutoka Nyanza,
Wagiriama wa Pwani,
Na vijana wa Kikalenjin,
Kuungana pamoja na Wakenya wengine,
Na kumfukuza kabisa adui.
Tumepeleka pia mabalozi Ethiopia kuchunguza ikiwa tunaweza kupata silaha. Lakini ni lazima nisisitize zaidi; kwamba jambo muhimu kuliko yote ni nguvu zetu wenyewe.
Hatuna budi kuendelea kutengeneza bunduki,
Nataka kuona kila kijana akiwa na bunduki.
Gurunedi,
Makombora,
Kila kambi, kila mbuci, iwe na kiwanda chake.
Hivi sasa tuna wahunzi hodari. Hata huwezi kutambua tofauti kati ya silaha zetu na zao.
Anzisheni viwanda vya nguo. Tuna bidhaa za kutosha, kutoka kwa magamba ya miti na ngozi za wanyama.
Tieni juhudi zaidi katika elimu:
Ardhi hii iwe ubao wa kuandikia
Lazima tujue historia yetu
Hasa vitendo vya wale
Waliokuwa wakipinga
Kuchukuliwa kwa nguvu Kenya yetu nzuri
Wale waliokuwa imara katika kupinga udhalimu na unyonyaji.
Naweza kuwatukuza mchana kutwa:
Waiyaki, Me Katilili
Mbatiani, Koitalel.
Na kuwalaumu wasaliti:
Mumias, Wang'ombe,
Karuri, Gakure,
Kinyanjui, Luka —
Wote waliotuuza kwa wageni kujinufaisha wenyewe na jamaa zao.
Lazima tujifunze kutokana na uwezo wetu wa zamani,
Udhaifu wa zamani

Kushindwa kwa zamani na
Ushindi wa zamani.
Pia limeni na kupanda
Papa hapa msituni
Ambapo tumefanya urafiki na ndege, nyoka na wanyama ambao hutuonya juu ya hatari ya adui.
Hapa tupande mbegu kwa kizazi kijacho
Papa hapa msituni, lazima tuangamize uwongo
Kwamba Mwafrika hakugundua chochote
Ondoeni udhaifu kama huo
Ulioingizwa kwetu kutokana na karne nyingi za ugandamizi.
Jitayarisheni, wafanya kazi na wakulima wa Kenya,
Ushindi wetu ni ushindi wa wafanya kazi
Ushindi wa wote duniani
Ambao wanapigana kujikomboa.
Lidumu Baraza la Ulinzi la Wananchi!

WOTE: Lidumu Baraza la Ulinzi la Wananchi!

KIMATHI: *[anabadilisha sauti]:*

Waleteni wakosaji,
Maadui wa mapambano yetu!
[huku watu wakienda kuwachukua, Kimathi aendelea na hotuba yake]:
Maadui wetu wana nguvu
Wanayo mabomu
Wanazo bunduki mathubuti
Uwezo wao ni mkubwa
Kwa nini niwafiche hayo?
Wana silaha nyingi mathubuti
Silaha za propaganda.
Redio, magazeti, shule,
Vyuo vyao vikuu wanapowafunza watoto wetu
Elimu ya kuzifanya akili zao dhaifu,
Elimu ya kuwafanya watumwa, waigaji na kasuku
Elimu inayowafanya kuwa vivuli badala ya watu halisi.
Lakini hata wao pia wana udhaifu
Udhaifu mkubwa usio kifani

Mapenzi yetu ya uhuru ndiyo risasi yetu
Ushindi wetu ndio gazeti letu
Lakini
Nguvu zetu kubwa kuliko bunduki zao mabomu na ujuzi wao
Tukiwa na umoja pamoja na nidhamu
Tunaweza tukahamisha milima
Tunaweza kumkomesha adui
Ukweli ndio bomu letu la *atomic,*
Lakini
Nidhamu ndilo bomu letu la *hydrogen*

WOTE: Adumu milele Jemadari wa wananchi!
Vidumu milele Vikosi vya Majeshi ya Wananchi!

Kimathi anafikiri sana kama ambaye amepagawa. Mbaria anamwendea.

MBARIA: Jemadari!

KIMATHI: Wako wengine:
Wale waliokwenda kushauriana na adui ingawa ni marufuku kufanya hivyo sasa.
Fahamuni kwamba mapambano yetu yanakabiliwa na pingamizi kubwa:
Upande mmoja unapendelea kujisalimisha na kutafuta mapatano
Kuunda koloni jipya ambapo tutakuwa si kitu.
Ni lazima tuwalaani!
Lazima tuwang'oe kati yetu

WOTE: Lidumu milele Baraza la Ulinzi la Wananchi!
Yadumu milele Majeshi ya Wapigania Uhuru!

Hungu, Gati, Gaceru, wanaletwa. Halafu baada ya muda mfupi, Wambariria, kaka yake Kimathi, analetwa akiwa amefungwa minyororo. Pole pole Kimathi anageuka na macho yake yanakutana na macho ya kaka yake.

KIMATHI: *[akiwa ameghafilika]:* Wambararia! *[anasita]:* Hata wewe, kaka yangu?

WAMBARARIA: Mimi ni . . . Nilikuwa. . . .

KIMATHI: Ndugu yangu mwenyewe — Kuniendea kinyume?

[anaketi]: Kimemia — niambie.

KIMEMIA: Jemadari, nakubaliana nawe kuhusu nidhamu
Nidhamu ya mtu binafsi.
Nidhamu ya watu wengi.
Nidhamu ya akili.
Nidhamu ya mwili.
Nidhamu njema ya kisiasa na kijeshi.
Sisi ni watu tunaopigana.
Mara nyingi umetuambia
Kuna wakati wa maneno na wakati wa kulaumiana.
Wakati wa mtu kujilaumu mwenyewe.
Huo ndio umekuwa mwenendo wetu.
[akiwageukia watu]:
Je, Kimathi amepata hata siku moja kumzuia ndugu yeyote asiseme atakalo?

UMATI: Laaaaaaaaaaaaaaaa!

KIMEMIA: Mwongozo wake siku zote umekuwa:
Zungumza, fanya mashauri, mpaka mapatano yafikiwe.
Lakini mara sheria zitungwapo,
Mara kazi zipangwapo,
Ni lazima zitiiwe
Mpaka watu wazibatilishe
Kutotii sheria hizo,
Ni kuangamiza juhudi zetu
Ni kama kuwahaini watu wetu
Ni kama kuwa na walinda majumba kati yetu!
Wasaliti hawa lazima wafe!

Ni kimya. Mikono mingi inanyoshwa na watu walio na hamu ya kuongea.

MPIGANAJI I: Wasameheni.
Ingawa wamefanya hivyo, hilo ni kosa lao la kwanza.
Kuwaua ni kupunguza idadi yetu.

MPIGANAJI II: Si idadi ipiganayo vita
Ni heri watu hamsini
Wenye imani na nidhamu njema

Kuliko wakorofi elfu nzima
Wenye shaka
Na ambao wanaweza kutusaliti.

MPIGANAJI III: Wamepigana kwa uhodari mwingi wakati uliopita.

MPIGANAJI: IV: Wakati uliopita ni historia, lakini itakuwa kosa kubwa kuwa watumwa wa historia!
Tusikubali ujasiri wa zamani utusalitishe juhudi zetu!
Tusikubali vitendo vya zamani kuwa msingi wa kuendelea kunyanyaswa na mabepari!
Hawa ni kina nani hata kuweza kutuwakilisha katika kujisalimisha kwa adui?

MPIGANAJI V: Mmoja ni ndugu yake Kimathi. Damu moja.
Hamwezi . . .
Damu itatugeukia
Na kutaka ilipizwe kisasi duniani.

KIMATHI: *[akimwota mwanamke]:*
Mnamwona huyu mwanamke? Amefanya mambo mangapi?
Tena bila kulalamika? Kati ya hapa na vijijini?
Amewaokoa wangapi kutoka gerezani!
Amewashawishi vijana wangapi kujiunga nasi?
Anatembea maili nyingi
Bila kulala.
Mapambano yetu yatakapofanikiwa
Tutajenga kumbukumbu kote mijini
Kwa heshima ya wanawake wetu
Kwa heshima ya mapambano yetu
Njoo mbele, mama yetu
Tufunze juu ya kujitolea
Wasemaje juu ya wazembe hawa?
Hawa wanaotusaliti?

MWANAMKE: *[anamtazama Kimathi halafu anaanza kusimama]:*
Nataka kusema neno
Kujibu aliyosema ndugu yetu
Kuhusu msaliti ndugu yetu! Kaka, mjomba, ndugu . . .
Mtajifunza lini?
Tutaendelea kutaabika

Hadi siku ile
Tutakapowagundua
Ndugu zetu wa kweli
Wakati tutakapoweza kuwatambua maadui zetu
Mawazo haya ya undugu ni ya nini
Ikiwa yanageuka na kutusaliti?
Ndugu zangu, ndugu zangu,
Kakangu, Dadangu,
Kama hawa ni wa nyumba yangu
Waheshimu ahadi za kiapo cha umoja
Waendelee na mapambano ya mkombozi, kutoka utumwani na kunyanyaswa.
Hivyo uamuzi wowote tutakaoufikia
Ni lazima uwe wa busara. Usitegemee damu ya ndugu.

UMATI: Lidumu milele Baraza la Ulinzi la Wananchi
Yadumu Mapambano ya Wananchi.

Kimya.

KIMATHI: *[akisimama kutoka pale alipokaa]:*
Wewe Hungu — Una lipi la kusema?

HUNGU: Ni kosa la kwanza. Nisamehe.

GACHERU: Ni kosa la kwanza. Nisamehe.

GATI: Ni kosa la kwanza. Nisamehe.

MWENDANDA: Tulitaka kujua watu wengi wanavyosema.

MPIGANAJI VI: Wote wana hatia. Lakini wapewe kazi mpya.
Sheria mpya.
Wakikosa kuzitii —

KIMEMIA: *[kwa hasira]:*
Halafu watoroke wamwendee adui
Nimetambua hayo mara moja.
Watatusaliti!
Ikiwa watafanya kosa jingine?
Wakiogopa hasira za wananchi?

KIMATHI: Na wewe Wambararia,
Unalo la kusema?

Wanatazamana kimya.

WAMBARARIA: Nimezisikia habari. Pia ninazijua habari mbaya.
KIMATHI: *[anageuka kwa kuudhika]:* Ondokeni nyote. Niacheni peke yangu.

Kila mtu anatoka nje ila mwanamke. Kimathi anabaki mahali papo hapo.

MWANAMKE: Najua inaumiza moyo.
KIMATHI: Hujui.
MWANAMKE: Babako aliuwawa katika vita vikuu vya kwanza.
KIMATHI: *[akumbuka]:* Nilikuwa mtoto tu.
Lakini nimesikia kwamba
Aliheshimiwa kote Karunaini.
Shujaa mkubwa.
Aliuwawa katika mapambano ya Tanga.
Na majeshi ya Wajerumani.
Lakini si hayo tu.
MWANAMKE: Kakako
Kakako mkubwa
Aliuwawa katika mapambano ya Mathari!
Alikufa katika mapambano yetu.
KIMATHI: Norman.
Gichuhi.
Kifo cha kishujaa.
Akipigania uhuru wa wananchi.
Namkumbuka daima.
Lakini si hayo tu.
MWANAMKE: Najua sana.
Ni dadako tu aliyebakia.
Lakini hivyo ndivyo ulivyopenda iwe.
KIMATHI: Mapenzi yangu.
Mapenzi yetu.
Damu yetu.
Damu ya damu yangu.
Tulizoea kucheza naye
Huko Karunaini
Katika kijito cha Theng'era

Tukizuru msitu wa Kabage
Mara nyingine tukipanda
Mlima Mathari
Tukaota ndoto juu ya nyanda za Nyeri
Na tukatunga ngano juu ya Mlima Kenya.
Siku moja kidole changu kilipokatwa
Katika kiwanda cha mbao
Ilikuwa Wambariria aliyekifunga kwa kitambaa.
Baada ya kuipasua shati yake mpya
Aah,
Inaumiza moyo sana
Haya sikani hata kidogo
Lakini si hayo tu.

Anatoa barua na kumrushia . . .

KIMATHI: Hii ndiyo ile barua uliyoniletea. Ilikuwa na habari mbaya sana. Ndani ya barua kutoka Muhoya lazima Wambariria awe aliisoma na kufahamu kwamba
Mama yetu sasa ameharibikiwa kichwa
Anachuma maua na kuimba
Akimwomba Mungu amwokoe Wambariria.
Amwokoe kitinda mimba wake —

Kimya — mwanamke anamrudishia Kimathi barua.

MWANAMKE: Inaumiza utu wangu pia!
Nikifikiria yaliyopita,
Wale tuliowaacha nyumbani
Wanaweza kudhoofisha dhamira yetu.
Wewe u kiongozi wa mapinduzi.
Ni lazima ukate shauri.
Lakini kumbuka pia wale wengine wamewaacha nyuma wake zao, watoto wao, mama zao.

KIMATHI: *[anatembeatembea]:* Nenda! Nenda uwaite.
Waambie warudi.
[Baada ya muda wote wanarudi.]

KIMATHI: *[akidhamiria]:* Rafiki, ndugu zangu katika mapambano.

Hili ni kosa lao la kwanza. Na ni kosa baya sana.
Lakini hatutamnufaisha fisi mara nyingine!
Safari hii wasinyongwe. Lakini wachapwe viboko.
Na wasipewe chakula kwa muda wa siku tatu.
Tutawachunga sana ipasavyo.
Tutachunguza vitendo vyao.
Ni lazima tuwaelimishe
Wapate dhamira ya mapinduzi. Lakini wakirudia kosa lao
Wakidiriki tu —

Wengine wanashangilia na wengine wamekasirishwa na uamuzi huo. Wote wanatoka nje. Kimathi anabaki jukwaani.

KIMATHI: Wanajeshi,
Kaeni chonjo,
Weni na nidhamu njema.
Kuna swala linisumbualo . . .
Mama yangu. . . .

Kimemia anarudi upesi jukwaani akifuatwa na mwanamke nyuma yake.

KIMEMIA: Jemadari! Jemadari!
KIMATHI: Sema.
KIMEMIA: Wambariria, Mwendanda, Gati, wote wamekimbia, wametoroka.
KIMATHI: *[kimya. Halafu anakata shauri]:*
Wafuateni hadi bondeni.
Waambieni Matenjagwo, Ole Kisio
Wafululize Mugumoini
Na njia panda nyingine.
Mkiwaona wapigeni risasi papo hapo!

Mahakamani, lakini sasa upande wa Wazungu kuna Waafrika wachache. Mwanasiasa, Mfanyi Biashara, Padri, Mwenye Benki, Gati, Gatotia, Hungu, Gaceru, Mwendanda. Wameketi juu ya ubao nyuma ya Wazungu. Hakimu yuko kitini. Kimathi angali na minyororo akilindwa kama pale mwanzo.

HAKIMU: Unashtakiwa kwamba usiku wa Jumapili tarehe 21 mwezi wa Oktoba, mwaka wa 1956, ukiwa Ihururu ama karibu na hapo, ulipatikana ukiwa na bunduki aina ya *revolver,* bila leseni, kinyume cha kifungu 89 cha sheria za nchi hii, jambo ambalo kulingana na hali ya hatari iliyopo nchini, ni kosa la jinai. *[Kimathi anawatazama wasaliti]:* Tunaye mwanasheria wa kumtetea mshtakiwa. . . .

KIMATHI: Wanasheria, Waongo, Wenye benki, Wenye Mali.

HAKIMU: Bila kupoteza wakati —

KIMATHI: Wakati ni mali. Mali ni haki. Haki ni mali. Haki ya mali. Vipande thelathini vya fedha. Majudas. Wasaliti.

HAKIMU: Wale?
Wamekuja kama mashahidi
Kushuhudia ukweli
Jinsi ulivyodhalimu
Jinsi unavyowadhulumu watu wako wenyewe!

KIMATHI: Ukweli kutoka kwa wakuu wa ukatili
Wauaji wa ukweli.

HAKIMU: Ukweli ni ukweli. Ni kama 2 + 2 = 4.

KIMATHI: 2 + 2 = 4? Inategemea msimamo wako.

HAKIMU: Unatetemeka. Unaogopa haki na ukweli?

KIMATHI: Naogopa? NAOGOPA! ONDOA WASIWASI HUO. ONDOA KABISA!

Anaingia mwanamke ambaye sasa amevalia nguo za kike. Kimathi anamtambua mara moja. Mara Kimathi anapata nguvu. Mwanamke anamtazama Kimathi. Macho yao yanakutana. Hakimu anamtazama mwanamke kwa makini. Mwanamke anakaribia kuketi, lakini mara kunatokea wasiwasi upande wa

wazungu. Anaketi na Waafrika walio mbele. Wasiwasi unaongezeka wakati wasaliti wanapoongea kwa sauti ya chini. Yote haya yanachukua sekunde chache.

HAKIMU: *[akigonga meza]:*
Kimya mahakamani!

Kimya.

HAKIMU: Kila mtu aliye hapa nataka afahamu kuwa mshtakiwa amekatalia mbali msaada wa mwanasheria uliotolewa na serikali. Sasa sina jingine, ila kuendelea na kesi, nikishikilia kuwa mshtakiwa atajitetea mwenyewe. Nitarudia mashtaka kwa mara ya mwisho. Mshtakiwa anashauriwa asikilize kwa makini na atoe utetezi wake.

Hakimu anapoendelea na mazungumzo hayo hapo juu, wasaliti wanashughulika zaidi na kuingiwa na hofu. Gaceru anazungumza na Gatotia na kumwita afisa mzungu wa polisi. Afisa anamwendea mwanamke. Anamtoa nje. Mwanamke anamtazama Kimathi. Anasukumwa, na anapotolewa anaanza kuimba wimbo wa uhuru na kujaza mahakama yote kwa sauti yake. Haya yote yanatendeka katika muda usiozidi dakika moja.

WIMBO:
Bururi uyu witu
Andu airu
Ngai ni aturathimiire
Na akiuga tutikoima huo.

Wanaingia mvulana na msichana — wamevalia kawaida na kuketi pale alipokuwa ameketi mwanamke. Wimbo wa mwanamke bado waendelea. Hakimu anajifanya kutoa amri kwa karani wa mahakama. Kimathi anawatazama msichana na mvulana mpaka wameketi chini.

HAKIMU: *[anajifanya ametosheka]:* Kimya mahakamani! Walinzi wahakikishe kuwa watu wanaokuja wamechelewa hawaruhusiwi kuingia ndani. Jambo hilo linaleta wasiwasi usiotakikana. *[walinzi Waafrika wanapiga saluti]:*
Dedan Kimathi bin Wachiuri, unashtakiwa kwamba usiku wa

tarehe 21 mwezi wa Oktoba, mwaka wa 1956, ukiwa Ihururu ama karibu na hapo, ulipatikana na bunduki aina ya *revolver*, bila leseni, kinyume cha Kifungu 89 cha Sheria za Nchi hii, jambo ambalo kulingana na hali ya hatari iliyopo nchini, ni kosa la jinai. Unakiri mashtaka ama la?

Kimya.

Kimathi anawatazama Hungu, Gati, Mwendanda na Gaceru. Wanatazama upande, kwa aibu.

HAKIMU: Kimathi bin Wachiuri, umepatikana na hatia ya kuwa na bunduki uliyopatikana nayo huko Ihururu ama karibu na hapo, usiku wa tarehe 21 Oktoba, kinyume cha Sheria Maalum za Hali ya Hatari. Una lolote la kusema kabla sijatoa hukumu?

KIMATHI: Katika mahakama ya kibeberu!
Hamjakuwa na hamtakuwa na
Haki sawa kwa wananchi
Walio chini ya ubwana huo.
Haki na usawa vinaundwa
Kutokana na mapambano ya mapinduzi
Kupinga uonevu wote na ubwana.
Mapambano yetu kwa hivyo yataendelea.
[Waafrika wanasimama. Kuna hali ya wasiwasi. Askari wanashikilia bunduki tayari]:
Msijielekeze kwenye mitutu ya bunduki
Kama nyinyi wenyewe hamna bunduki!
[anaendelea na hotuba yake]:
Msituni nilijawa na mashaka.
Nilikuwa nikijiuliza:
Kama leo nikiaga dunia
Wananchi wetu wangeendelea na mapambano?
Nilikuwa nikiwatazama mashujaa waliouawa na adui
Nikajiuliza tena:
Kama leo nikiaga dunia
Damu hii ingelipiwa thamani yake?
Hayo yalikuwa majaribu yangu.
Lakini sasa ninatambua kuwa

Kwa kila msaliti mmoja
Kuna mashujaa elfu moja.
[anawatazama wasaliti, na kila mtu anatazama upande huo]:
Kwa ishara ya Hungu, Gati, Gaceru, Mwendanda,
Wakiongozwa na Gakunia,
Aliyewahaini mamia ya wazalendo wanaopambana,
[mshangao upande wa Waafrika]:
Mtumishi wa sheria zenu za ubwana
Ambaye sasa hivi alimburuta mwanamke mzalendo wa mapambano,
Mzalendo halisi,
Kwenda kuuawa na adui.
[anatazama upande mwingine kwa dharau na karaha]:
Lakini mfahamu kuwa watu wetu hawatajisalimisha
Maadui wa nje na ndani
Wote wataangamizwa
Na Kenya itakuwa huru!
[Waafrika wanashangilia.]

HAKIMU: Kimya mahakamani!

KIMATHI: Basi sasa nendeni!
Mkajitayarishe mijini na milimani
Mfahamu kuwa ndugu yenu halisi ni yule
Aliye katika mapambano
Walaanini
Wale wanaodhoofisha mapambano yetu
Kwa kuunda ukabila
Waondoeni wale wanaoshawishiwa na ubeberu
Wananchi wa Kenya watakuwa huru!

HAKIMU: Kimathi bin Wachiuri, unahukumiwa kufa.
Utanyongwa kwa kamba hadi ufe.

KIMATHI: *[anacheka.]*

Kila mtu anasimama. Mara hakimu anapotoweka, mvulana na msichana wanasimama. Wakitembea kwa haraka kuelekea aliko Kimathi, mara msichana anauvunja mkate na kushika bastola.

MVULANA NA MSICHANA: Hatakufa! *[msichana anajitayarisha kupambana na walinzi.]*

Kuna ghasia kati ya pande mbili zinazohusika. Mara kunasikika mlio wa bunduki iliyofyatuliwa. Kwa muda kidogo kuna giza, lakini mara moja wanaonekana waafrika wafanyakazi na wakulima, pamoja na mvulana na msichana wakiimba wimbo wa mapambano. Askari wote wameondoka isipokuwa Askari wa Kwanza Mwafrika ambaye naye anajiingiza katika shughuli hizo.

Wimbo wa wananchi na ngoma:
Viongozi wa kike na wa kiume wangefaa sana.

VIONGOZI: Ho-oo, ho-oo mto mkuu wateremka!
WATU: Ho-oo, ho-oo mto mkuu wateremka!
VIONGOZI: Magharibi kwenda mashariki
WATU: Mto mkuu wateremka
VIONGOZI: Kaskazini kwenda kusini
WATU: Mto mkuu wateremka
VIONGOZI: Hoo-i, hoo-i kumbe adui kweli mjinga
WATU: Hoo-i, hoo-i kumbe adui kweli mjinga
VIONGOZI: Akaua mwanza mimba wetu
WATU: Akijitia yeye mshindi
VIONGOZI: Wengi zaidi wakazaliwa
WATU: Tushangilie mazao mapya
VIONGOZI: Vitinda mimba marungu juu
WATU: Tushambulie adui mpya.
VIONGOZI: Hoo-ye, hoo-ye wafanyakazi wa ulimwengu
WATU: Hoo-ye, hoo-ye wafanyakazi wa ulimwengu
VIONGOZI: Na wakulima wote wadogo
WATU: Tushikaneni mikono sote
VIONGOZI: Tutwange nyororo za wabeberu
WATU: Hatutaki utumwa tena.
VIONGOZI: Hoo-ye, hoo-ye umoja wetu ni nguvu yetu
WATU: Hoo-ye, hoo-ye umoja wetu ni nguvu yetu

VIONGOZI: Tutapigana mpaka mwisho
WATU: Tufunge vita na tutashinda
VIONGOZI: Majembe juu, mapanga juu
WATU: Tujikomboe tujenge upya.



NGUGI wa THIONG'O ni mwandishi wa vitabu vifuatavyo katika mfululizo maarufu wa Waandishi wa Kiafrika: *Usilie Mpenzi Wangu (Weep not, Child), Njia Panda (The River Between), A Grain of Wheat* na hivi karibuni, *Petals of Blood.*

Michezo yake ya kuigiza Wakati Kama Huu Kesho (This Time Tomorrow), Mtawa Mweusi (The Black Hermit) imemwimarisha kama mwandishi mashuhuri wa michezo.

Mpaka hivi karibuni, Ngugi alikuwa Mwenyekiti wa Idara ya Fasihi katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

DK. MICERE GITHAE MUGO amekuwa akiandika toka 1962. Baadhi ya kazi zake zimepata kutangazwa katika Idhaa ya BBC na zimechapishwa katika magazeti na majarida mengi ya fasihi. East African Literature Bureau wamechapisha kusanyiko lake la mashairi, *Daughter of My People, Sing;* mchezo, *The Long Illness of ex-Chief Kiti* na kitabu kimoja cha *Visions of Africa*. Micere Githae Mugo amehusika sana katika michezo ya kuigiza toka alipokuwa na umri wa miaka minane. Kwa sasa ni mwalimu katika Idara ya Fasihi ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Yamesemwa na kuandikwa mengi juu ya kiini cha mapambano ya Mau Mau na vikosi vya Wakoloni Waingereza. Lakini je, kiini hiki kimezungumziwa vya kutosha katika fasihi ya Kenya? Ni kwa nini fasihi hii imewadunisha wazalendo na kuwafanya wasioweza kuiunda historia yao? Kwa nini waimbaji wetu Kenya hawajapata kuimba nyimbo za kuwasifu mashujaa kama Dedan Kimathi na ujasiri wao? Historia na matendo waliyoyaandika wanahistoria na waandishi wengine ni vya nani? Haya ni baadhi tu ya maswali yaliyowafanya Ngugi wa Thiong'o na Micere Githae Mugo kuuandika mchezo wa *Mzalendo Kimathi,* mchezo wa aina ya pekee unaoonyesha mapambano ya Kenya katika kujikomboa. Mhusika mkuu ni Kimathi, kiongozi shupavu wa mapinduzi ya Mau Mau. Ingawa anateswa kwa njia nyingi, Kimathi anagoma kabisa kujisalitisha na Ubeberu wa Waingereza.

Mchoraji: Patrick Tumwine